# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## Verbatim Report of

## DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL,

## ELDORET EAST CONSTITUENCY

## T.A.C. (CENTRAL PRIMARY SCHOOL)

## ELDORET TOWN

ON

17TH OCTOBER 2002

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, ELDORET EAST CONSTITUENCY T.A.C. (CENTRAL PRIMARY SCHOOL, ELDORET TOWN ON 17TH OCTOBER 2002**

**Present**

1. Salome Wairimu Muigai - Commissioner

**Secretariat Staff in Attendance**

1. Dan Juma - Assistant Programme Officer
2. Asenath Kanga - Verbatim Recorder
3. Glbert Bor - District Coordinator

The meeting started at 12.45 a.m with Commissioner Salome Wairimu Muigai in the chair.

**Gilbert Bor:** Tuko tayari sasa kuanza mkutano wetu sasa ningeomba mmoja wetu atulinde kwa maombi….(Inaudible)

**Prayer:** Tuombe. Mwenyezi Mungu tunakuja mbele zako wakati huu hasa kama mfanyikazi nashukuru Mungu kwa sababu …(Inaudible). Kwa kutenda kazi ambayo Mungu tunakuweka mbele ili akaenda kutuongoza katika kazi yako hata tunapoanza mkutano huu ukaweza kuwa pamoja nasi hadi tutakapomaliza. Tunakushukuru na tunasema asante kwa sababu uko pamoja nasi na ni katika jina la Yesu tunaomba na kuamini. Amen.

**Gilbert Bor:** Ningeomba wale members wa Constitutuency Committee tafadhali mje hapa tukapate kuwajua. Vile vile tuko na delegate mmoja tungali zote tutakuja kumjua.

**Samuel Sigoti:** Jina langu ni Samuel Sigoti mimi ni Committee Member kutoka Eldoret East.

**Speaker:** Committee member kutoka Eldoret.

**Benard Mutai:** Mimi ni Benard Mutai, Committee Member, Eldoret.

**Ruth Kemboi:** Mimi ni Ruth Kemboi, Committee Member kutoka Moiben – Eldoret East.

**Gilbert Bor:** Vile vile nimeona mnajua tuna district delegates' ambao wataenda kwa National Conference kuakilisha wilaya hii, mmoja ndio huyu atajitambua.

**Julius Sietenei:** Madam Commissioner pamoja na district Coordinator …(Inaudible) Wananchi watukufu hamjambo, majina yngu ni Julius Sietenei, mimi ni mwalimu nitawakilisha wilaya hii. Asante.

**Gilbert Bor:** Vile vile mnajua mimi ni District Coordinator Uasingishu na ofisi yetu iko katika library, wengi wenu mnajua na siku hii ya leo ni kufanya lauching ya draft Constitution.

**Com. Salome Muigai:** Hamjambo mabibi na mabwana?

**Audience:** Hatujambo.

**Com. Salome Muigai:** Kwa niaba ya Tume ya Kurekebisha Katiba ya Kenya ningetaka kuwalika kwenye kikao hiki ningetaka pia kuomba radhi kuwa mkutana ilianza kama tumechelewa na pia tunahitaji watu wengi kuwa tukiwa na kikundi kama hiki sio haki ama sisi watu wa Eldoret East ni hawa tu. Ni watu hawa pake yao, kwa hivyo tulikuwa tukijaribu tukienda hapa na pale kuona kama tunaweza kupata kikundi kikubwa cha watu ili kuelewa tunafanya nini siku ya leo. Ningetaka kwanza kuwajulisha wenye tumekuja nao kutoka Nairobi, kwa upande wangu wa kushoto nitamwacha ajitambulishe mwenyewe kwani yeye ni mwandishi na hamtapata nafasi nyingine ili msikie sauti yake. Mngetaka kusikia sauti yake? Okay, sasa tuendeleee.

**Dan Juma:** I am Dan Juma…(Inaudible)

**Com. Salome Muigai:** Asante Bwana Juma pia upande wangu wa kulia tunataka mwenye kalamu na yeye atajieleza jina lake,

tafadhali.

**Asenath Kanga:** Habari zenu, kwa jina naitwa Asenath Kanga mimi ndio nitakua nachukua recordi ya kila kitu yenye mtakuwa mnasema nitafanya recording ya hii proceeding. Asante.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana Bwana Juma na mwenzake Kanga. Sasa na mimi mwenyewe naitwa Salome Wairimu Muigai na nafurahi kuwa hapa kwa ajili mimi ni local girl nimezaliwa hapa na nilisomea Township School na Mr. Kasurai hapa atakumbuka alinifundisha nikiwa Standard Five, sasa ningetaka kueleza ….juu ya Tume. Tume hii ya marekebisho ya Katiba iliwekwa pamoja na Act of Parliament kama vile mlivyojua na kazi ile maalum ilikuwa ni kuchukua maoni yenu na kuyaweka pamoja na kuandika repoti. Tulikuja tukachukua maoni kadha hapa na tukaandika ilo repoti na sijuhi kama wengi wenu mlikiona hili nakala ilikuwa kwenye gazeti, tuliandika repoti ya "The People's Choice" na tukaiweka kwa gazeti, hiyo sasa ndio ilikuwa kazi yetu hii ilikuja volume moja ya hizo tatu na tuliweka kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Ya Kiswahili iliandikwa Chaguo la Wananchi na ya Kiingereza iliandikwa The People's Choice.

Halafu kazi yetu ya pili ilikuwa ni kuandika mswada wa ule Katiba na huo mswada pia tumeuandika tukauweka kwenye gazeti pia na kwanza tulitoa kwa Kiingereza, draft Constitution of the Republic of Kenya hivi ama mlipata kwa gazeti.

**Speaker:** …(Inaudible)

**Com. Salome Muigai:** Kama tumeshapeana, kila mtu ameiona hiyo nakala. Kila mtu amekaa pale anaweza kuliangalia make sure you are sitting where you can see a copy na ukiwa hauoni uulize Bwana Bor atupe zaidi tuokoe wakati au unaweza kukaa pahali ambapo unaweza kuliangalia.

Sasa kazi yangu leo ni kazi kidogo sio kama ya kuchukua maoni. Mmemaliza kupeana? Tulikuja Eldoret East ama Eldoret ya nini, East ni gani?

**Speaker:** Eldoret Mashariki.

**Com. Salome Muigai:** Mashariki, Kikao cha Bunge cha Eldoret ya Mashariki na mkatupa maoni. Siku ya leo basi tuliangalia mswada wa kwanza yenye tumeutengeneza tukaona kama pia mambo yenye tulichangia ama mambo yenye tulikuwa tunataka kuanayo kwa hii Katiba kama tumechukua maoni yenu. Leo kazi ni kufanya launching, ni kufanya introduction na launch yaani ni kuwatanguliza tu kwenye hii Katiba, hatuwezi kulisoma neno kwa neno kwani tuna muda mfupi. Hii ni Katiba yenye utachukua siku nyingi kuisoma bila kufanya kazi ingine, ikiwa wewe ni mtoto … utachukua masaa fulani, ikiwa wewe ni mtoto wa …. Utachukua wiki moja hivi kwa hivyo hatutasoma neno kwa neno lakini ningetaka kuwapatia introduction ama utangulizi na kuelezea ili nawe ukienda nyumbani uweze kujisomea ama wewe ukiwa ni baba ama mama na uwezi kusoma pengine

umuulize mtoto ama mtu mwingine rafiki yako aweze kukusomea.  Ukishasomewa ningetaka umweleze mtu mwingine juu ya haya mambo ni kama bibilia, ukisikia maneno, inaitwaje, good news.  Maneno…

**Speaker:** Habari njema.

**Com. Salome Muigai:** Habari njema, ukisikia habari njema ni lazima ufanye nini?  Ujulishe wengine si hivyo, si vizuri kujua mwenyewe mtu akiwa peke yake itakuwa na …. Kwa hivyo ningetaka tafadhali tusikize kwa makini mkiwa na maswali nitawapa nafasi nikishamaliza muulize mswali halafu nitalizungumzia na …

Tukitazama ukurasa wa pili, kila pahali penye tulienda kulikuwa na mambo mengi yenye Wakenya walikubaliana.  Moja yake ni kuwa Katiba yetu ya sasa haina utangulizi yaani preamble na kila mtu alisema, watu wengi zaidi walisema ni vizuri Katiba kuwa na preamble.  Basi sasa Katiba yetu ina-preamble unaiona hiyo preamble kwenye ukurasa wa pili.  Hii preamble inaanza kwa kusema ni nani mwenye kutengeneza Katiba na inasema ni nani mwenye kutengeneza Katiba?  Wanasema ni nani?

**Audience:** Watu wa Kenya.

**Com. Salome Muigai:** Sisi nani?

**Audience:** Sisi watu wa Kenya.

**Com. Salome Muigai:** Sisi watu wa Kenya ama sisi wananchi wa Kenya.  Tukifahamu wingi wa tofauti zetu za kikabila na za nini tena?  Za kidini na ni za nini tena?  Waalimu tusaidieni kwa lugha.  Tukifahamu wingi wa tofauti zetu za kikabila, kitamaduni na kidini na tukidhamiria kuishi kwa nini?

**Audience:** Kwa amani.

**Com. Salome Muigai:** Kwa amani na umoja kama taifa moja huru lisilogawanyika.  Tukijitolea kufanya nini, kulea na kufanya nini, na kulinda ma majukumu za nini masilahi ya nani.  Ya kila mmoja, ya familia na pia ya nini?  Ya jamii katika hili taifa letu. Tukitambua matumaini ya nani?

**Audience:** Ya akina mama.

**Com. Salome Muigai:** Ya akina mama,  hiyo ndio tafsiri ya ….

**Audience:** Ya wanawake.

**Com. Salome Muigai:** Ya wanawake na nani.

**Audience:** Na wanaume.

**Com. Salome Muigai:** Na ya wanaume wetu ya kuwa na serikali ambayo imejengwa katika misingu muhimu inayodhamini nini?

**Audience:** Uhuru.

**Com. Salome Muigai:** Uhuru, nini tena, demokrasia, nini tena?

**Audience:** Haki ya kijamii.

**Com. Salome Muigai:** Haki ya kijamii na utawala wa sheria. Tukitekeleza haki yetu isiyojengeka ya uhuru ili kuamua aina ya utawala ama nini? Utawala ama serikali, si hivyo. Government ambayo imejengwa, sorry. Utawala wa nchi yetu na tukiwa tunashiriki kikamilifu katika nini? Utaratibu wa kufanya nini? Wa kuandaa ama kuunda katiba, tunaifanya nini hii Katiba. Tunaikubali, tunaifanya sheria na tunaipeana kwetu wenyewe na kwa vizazi vyetu vijavyo Katiba nchi, yaani hi Katiba tunampa nani? Tunajipatia sisi wenyewe, si hivyo na tunajipa wakati huu na wakati gani mwingine.

**Speaker:** Ujao.

**Com. Salome Muigai:** Na wakati ujao, hii Katiba tunaanzia hivyo na tunasema Mungu afanye nini?

**Speaker:** Mungu aibariki Kenya.

**Com. Salome Muigai:** Mungu ibariki Kenya, hiyo ndio utangulizi wetu kila mtu alisema tuanzishe utangulizi. Tunakubaliana na huo utangulizi.

**Audience:** Ni sawa.

**Com. Salome Muigai:** Kuwa imewekea maanani matako yetu ama maoni yetu? Mkinyamaza ni kusema ndio ama ni kusema hapana.

**Audience:** Ni sawa.

**Com. Salome Muigai:** Ni sawa basi hiyo ndio utangulizi wetu. Tukiangalia kwenye sura ya kwanza hii Katiba inasura ishirini kwa hivyo kwa sababu tunaanza saa saba ni wakati wa njaa tutaenda speedy lakini nitajaribu kutumia masaa mawili ama masaa mawili na nusu tutembee kila pahali kutoka sura ya kwanza mpaka sura ya nini? Ya ishirini ndio ukienda kuulizwa na mtu mwingine, ulienda kwenye mikutano wa Katiba uweze pia kufanya nini, kumueleza ulienda na ulisikia nini na ikiwa na maswali uweze kumfanya nini, kumjibu.

Tukiangalia sura ya kwanza inazungumzia juu ya uhuru kwa wananchi na ukuu wa Katiba, the sovereignty of the people and the supremacy of the Constitution. We want to know tunapozungumzia uhuru wa wananchi hiyo inamaana gani, inakueleza uhuru wa wananchi una maana gani. Inasema mwanzoni, uhuru wa wananchi mamlaka yote ya uhuru ni ya wananchi wa Kenya na yanaweza kutekelezwa tu kulingana na Katiba. Inasema pia kuwa wananchi watatekeleza, ukiangalia ukrasa wa nne na ukiwa unasoma daraja ya Kiingereza usijali hiyo yenye tunasoma kwa Kiswahi ni yale yale uliyoko ndani katika Kiingereza ama mnataka tusome na Kiingereza. Mnataka lugha gani?

**Audience:** …(Inaudible).

**Com. Salome Muigai:** Na wale wenye hawajuhi lugha hii mnataka lugha gani? Ya Kikikuyu.

**Speaker:** Kiswahili.

**Com. Salome Muigai:** Okay tujiadhari sana, okay Kiswahili.

Wananchi watatekeleza uwezo wao uhuru kwa njia ya moja pamoja au kupitia kwa wakilishi wao watakaochaguliwa kidemokrasia na pia inaendelea kueleza mengi juu ya hiyo, hatutasoma moja kwa moja kwa undani sana lakini hio ni introduction tu. Tafadhali ukitaka kujua mengi endelea kufanya nini, kuisoma. Inazungumzia pia ukuu wa Katiba, Katiba yetu inaukuu upi? Inasema kuwa Kenya imejengwa katika msingi wa ukuu wa Katiba na utawala wa sheria na itatawaliwa kwa muujibu wa nini, wa Katiba. Katiba ndio sheria kuu zaidi na tunajifunza tawala zote na watu wote kote katika nini, jamburi ama taifa, hakuna mtu mwenye ataenda kinyume cha Katiba na ukienda kinyume cha Katiba itakuwa ni haki?

**Speaker:** La.

**Com. Salome Muigai:** Itakuwa sio tena halali. Upande huu sisikii mkiniambia kama… najua kuna wenzetu wenye hawasikii pia na wanaona kwa ishara ndio watu wenye wako upande huu ama kuna wengine wenye wanatumia kwa masikio**.** ***(Laughter*** ) Kuna wengine wanatumia masikio, tafadhali basi tumia masikio na tutumie midomo yetu ili tuweze kuwasiliana. Mimi ni mwalimu sijazoea kujizungumzia mimi mwenyewe tu, nimezoea kuzungumza na watu, kushauriana kwa ajili hii ni mashauriano hii

si kitu ya dakika saba, dakika ishirini mlale kidogo mnaamshwa na kiti kikisongeshwa ndio tuondoke. Ningetaka kila mtu aweze kusikiliza na kila mtu awe macho ili tufanye nini, tuwasiliane. Kwa hivyo tunasema Katiba yetu ndio sheria kuu ya nchi gani? Nchi yetu halafu tunasema vile Katiba itakavyotekelezwa, utekelezaji wa Katiba. Tunazungumza pia juu ya ulinzi wa Katiba, kwa nini Katiba inahitaji kulindwa? Kwa sababu Katiba ndio haki ya kila mmoja, kwa hivyo wale watu wenye wangetaka kukeuka haki za mtu mmoja angetaka kuvunja sehemu ya Katiba, kwa hivyo yule yeyote yeye ni Mkenya na anataka kulinda haki zake na za mwenzake ni lazima afanye nini? Alinde nini, alinde Katiba.

Tumezungumzia juu ya sheria za Kenya, zenye tumeuliza Kenya inasheria zinatoka wapi. Sheria ya kwanza ya Kenya tumekubaliana ni nini? Ni Katiba. Tutakuwa pia na sheria zenye kuundwa Bungeni. Wakati mwingine tutaangalia pia sheria za kitamaduni kulinganisha na mambo tofauti kama habari ya ndoa, habari ya huhusiano kati ya mimi pengine na jamii yangu. Tutaangalia pia sheria zingine za kidini wakati mwingine hasa katika dini ya Kiislamu yenye imeeleza wazi vile wataishi. Tutaangalia pia habari ya common law, sheria zenye zinajulikana kuwa ingawa Katiba haijasema usinitukana kila mtu atajua ukinitukana hiyo ni makosa ama ni wazi, ni makosa lakini ina mahali imeandikwa? La. Kwa hivyo kuna sheria zingine zenye tunaelewa ingawa hazijaandikwa kuwa ni sheria za mazoezi. Ya, common law we understand them although they may not be sometime written na pengine hazijaandikwa chini.

Halafu ya pili, inaangalia habari ya Jamhurii inaanza kwa kutangaza kuwa Kenya ni nini, ni Jamhurii. Kama Kenya haingekuwa ni Jamhurii inaweza kuwa nini tena? Kitu gani ingine yenye rules zenye pia Jamhurii inakuwa kama Wingereza ni nini? Ni milki si hivyo, wana malkia ama mfalme kwa hivyo hiyo ni milki. Kama Somali hakika kweli wanazungumza hawa hawana Jamhurii wana nini? Wana uchafuko pia hiyo ni serikali, hiyo ni nchi, si hivyo kuwa wanajua wanauchafuko usio na serikali bado tunajua basi Somali haiko si hivyo. Kwa hivyo sisi wenyewe kama Wanakenya tutatangaza kuwa nchi ni nini, ni Jamhurii. Na pia tumeeleza sehemu yetu, mipaka yetu iko wapi, ikiwa ni Jamhurii ama ni nchi fulani lazima tuelewe kuwa Jamhurii yetu inaanza hapa, inakomea pale.

Imeeleza pia habari makao yetu makuu, tumesema makao makuu ni wapi? Ni Nairobi, imeeleza pia habari ya lugha, sisi katika Jamhurii yetu tumesema tuna lugha za taifa na tuna lugha mbili rasmi. Lugha mbili rasmi ni gani na gani?

**Audience:** Kiswahili na Kiingereza.

**Com. Salome Muigai:** Ki- Turkana na nini tena?

**Audience:** Ooh, Kiswahili. Kiswahili na nini, na Kiingereza na lugha yetu ya kifaifa je, ni Kiswahili. Tumeeleza pia kuwa taifa letu ama Jamhurii yetu sio taifa ya kidini yaani haina dini la taifa lakini dini zote zitapewa usawa kwenye Katiba. Jana nilisoma sijui kama wengine walisoma wakiuliza kama dini zote zimepewa usawa kwa nini basi tuna koti ya Kiislamu na hatuna koti ya …

**Audience:** Ya Kiikristo.

**Com. Salome Muigai:** Ya Kikristo, wao huenda kotini kama ni Mkristo na unaapishwa kwa nini.

**Audience:** Kwa Bibilia.

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo nyinyi kusikia kuwa kuna nini kwenye koti, kuna ofisi ya Kiislamu lakini mbali na hiyo ningetaka pia kueleza vile ilikuja kwa ajili ya historia. Ukikumbuka wakati tulipopata uhuru kipande kikubwa cha mile kumi katika Mkoa wa Pwani kilikuwa sio cha nchi ya Kenya, kilikuwa cha Sultan. Kwa hivyo mashauri yenye ilikubaliwa kati ya Sultan wa wapi?

**Speaker:** Zanzibar.

**Com. Salome Muigai:** Ilikuwa Sultan wa Zanzibar ndio …..

**Speaker:** Oman

**Com. Salome Muigai:** Oman, basi wananchi hawa wako wapi, haya huyo ni Sultan. Makubaliano yenye ilikubaliana tulikubaliwa kati ya Kenya na Sultan ni kuwa Waislamu watakubalishwa kuwa na koti yao ili waweze kufanya sheria yao ya kibinafsi. Tofauti ya sheria ya kinafsi na ile ingine tulisema, sheria ya kibinafsi ni yenye inahusisha kwenye wewe na jamii yako habari ya viwanda, ya kuzaliwa mtoto, ya kurithi, ya talaka, mambo kama hayo. Yaani sheria ya kibinafsi, personal law. Waislamu wanakubalishwa kufuata personal law mradi tu isigeuke nini, Katiba. Ni vile pia sisi tunakubalishwa kufuata kitamaduni, si ndio, ukiolewa kitamaduni hiyo ndoa yako inakubalika kwenye serikali lakini unakubalishwa kitamaduni mradi tu isigeuke nini, Katiba ama sheria zenye zimeandikwa. Kwa hivyo ….(Inaudible)

Haya, tumesema pia dini zote zitapatiwa usawa hakuna dini yenye itakuwa na mamlaka kubwa kuliko nyingine kwenye taifa hili ama Jamhurii yetu na tumesema pia kwenye Jamhurii yetu tutakuwa na alama fulani yenye kuonyeshana ni za Jamhurii ya Kenya. Alama ya kwanza ni nini?

**Audience:** Bendera.

**Com. Salome Muigai:** Bendera yetu ndio alama ya kwanza, alama ya pili?

**Audience:** Wimbo wa taifa.

**Com. Salome Muigai:** Wimbo wa taifa, alama ya tatu?

**Audience:** Court of arms.

**Com. Salome Muigai:** Nimeambiwa kuwa Court of Arms inaitwa nembo, sisi zote tunarudi tu kwa lugha. Halafu pia tuna nini tena, tuna mhuri wa taifa si hivyo? Hiyo ni mhuri inaitwa mhuri wa taifa la Kenya. Halafu pia tumeweka viapo yenye tutaapisha watu wenye tutawapatia mamlaka ya kutulinda. Mimi nitaomba radhi kwa kunyua maji, waalimu wote wanajua kuwa ukizungumza kwa muda mrefu unakauka koo hata sio waalimu tunajua hivyo. Pia kuna viapo vya taifa na matamko ya dhati wale wenye hawaapi, kila mtu ukiwa mahakimu wenye tutachagua hata nani mwengine mwenye tunamwapisha, Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri wetu, Mawaziri Wadogo, Majaji na kila mtu. Kwa hivyo kwenye hii Katiba kuna ile kiapo yenye tutawaapisha hawa wenye kuchukua uskani wa mamlaka ya nchi hii.

Sura ya tatu inatueleza juu malengo ya taifa na maadili na kanuni, nini hizo kwa Kiingereza, what are they? Personal goals, values and principles basi ni hayo wenye lugha wanasema hiyo ni malengo ya taifa maadili na kanuni na hiyo iko katika ukrasa nambari kumi na nne. Inaseme malengo ya taifa, madili na kanuni nambari ya kwanza, malengo ya taifa, madili na kanuni zilizoko katika sura hii zinahusu mamlaka ya nchi, mamlaka ya nini tena, ya Bunge, ya mahakama, ya tawala za wilaya na vyombo vingine vya serikali na viongozi, raia na muungano ya nini, ya kibinafsi pale ambapo chombo kimoja kitafanya jambo hili ama lingine. Kwanza kama tunatumia na kuifafanua Katiba au sheria zinginezo. Pili, kama tunatumia, tunaunda na kutekeleza madili ya sera. Sera ni nini? Policy.

Halafu ningetaka kusoma nambari moja ama mbili. Ya kwanza, Jamhurii itaguuza umoja wa taifa na kuendeleza hali ya kujitolea kwa raia wake kwa mwito wa nini, wa utaifa. Ya pili, Jamhurii itatambua wingi wa tofauti wa wananchi wake na kuguuza tamaduni za jamii zake. Nne, Jamhurii imejengwa katika misingi ya kanuni ya kidemokrasia na itaendeleza ushirika wa wananchi katika maswala ya taifa na kuhakikisha ugawaji na upunguzaji na uzambazaji wa nini, wa madaraka. Yaani ugawaji wa kila madaraka hatuawekwa kwenye pahali pamoja, utazambazwa na kutawanywa, tunaelewa? Basi tumesema hayo na hayo mengine mtajisomea lakini kabla sijatoka kwenye hiyo sura ningetaka kusoma nambari kumi na moja. Inasema hivi, Jamhurii itahakikisha kushiriki kikamilifu kwa wanawake na nani mwingine, walemavu, jamii zilizowekwa pembeni na sector za jamii katika maisha ya nchi, katika mipaka ya jamii na nini, na kiuchumi. Yaani which people have free ni nini?

**Audience:** The people's rights.

**Com. Salome Muigai:** The people with disabilities, who else?

**Audience:** Women.

**Com. Salome Muigai:** Women, who else?

**Audience:** Marginalized groups.

**Com. Salome Muigai:** Marginalized groups hiyo ni moja ya dhamana ya Katiba yetu mpya.

Nambari kumi na mbili inasema hivi, serikali itatekeleza kanuni kuwa kikundi moja ya wanachama wa vyombo vyote inavyofanyiwa uchaguzi na uteuzi ni nani?

**Audience:** Ni wanawake.

**Com. Salome Muigai:** Ni wanawake, kwa hivyo tukiwa na watu thelathini kwenye kikundi lazima watu wangapi wawe wanawake?

**Audience:** Kumi.

**Com. Salome Muigai:** Kumi. Nambari ya kumi na tatu. Jamhurii itatambua majukumu maalum ambayo ni taifa, jamii na wazazi wa nani? Kwa watoto wetu na itahakikisha kuwatumikia mahitaji yao ya hali na nini, na mali yaani dhamana ingine ni kuhusu watoto wetu. Kwanza watoto wetu ndio nini, our children are our future aren't they? Watoto wetu ndio nini, ndio serikali tusipowachunga watoto tutakaa kwa vizazi vingapi ndio tuishi? Si tutakwisha tu …(Inaudible). Basi hizo ndizo dhamana zimeendelea mingi zaidi tafadhali zisome uelewe.

Sasa pia baada ya malengo tuna wajibu wa raia, hiyo inaitwa nini kwa Kiingereza? Duties of a citizen na raia anawajibu fulani, wajibu wa kwanza ni nini? Ili kutimiza malengo ya kitaifa, madili na kanuni raia wote wanawajibu wa kwanza, kujifahamisha kuhusu masharti ya Katiba na kudumisha, tunaelewa hiyo. Na kudumisha nini, maadili na malengo yake. Pia raia ako na wajibu mwingine wa kutetea na kufanya nini, na kuilinda Katiba na sheria. Mwanakenya pia anawajibu wa kutekeleza haki yao ya nini, ya demokrasia kwa kupiga kura na kushiriki katika namna zingine na shughuli za nini, za kisiasa. Una wajibu, mnaelewa wajibu ni nini? Tumasema kwa Kiingereza ni nini, duties na neno nyingine la kuwa katibu ni nini, ni jukumu. Ni jukumu langu kama Mwanakenya, kwa hivyo tutaendelea pia kuangalia jukumu gani ingine chenye wananchi wamewekewa.

Sasa tuende sura ya nne. Mkitaka tukakubaliane tutakuwa na mikutano mingapi kwenye hii mkutano, tutafanya Katiba yetu. Je, tutakuwa na mikutano mingapi na mwenye ataanzisha mwingine nitafanya nini naye? Tutamwonya, tafadhali basi tusianzishe mkutano mwingine humu humu.

Sura ya nne inazungumzia juu ya nini, ya uraia. Imesema kanuni za kijumla kuhusu uraia vile unaweza kudumisha uraia wako, vile unapenda kupata nini, uraia. Inazungumzia pia habari ya uraia wa nini, wa kuzaliwa na uraia wa nini tena, wa ndoa na uraia wa kujiandikisha. Inazungumzia pia vile tutakavyofanya na watoto wanaopatikana Kenya na watoto wa kando, yaani watoto wenye tumewapata na hakuna haki wamepewa. Tumesema kuwa mtu yoyote atakaye patikana hatutaki kusema tunaokota watoto kwani mnaokota nini. Hawawezi wakasimama kama takataka, kwa hivyo hatutaki kusema mtoto amefanya nini, ameokotwa. Kwa hivyo tunasema ikiwa mtoto yoyote atakayepatikana Kenya akionekana kama ana umri wa miaka nane, kwa nini hatusemi akiwa na miaka nane. Kwa nini Katiba haisemi akiwa na miaka nane inasema akionekana kama ana miaka nane? Kwa sababu hatutajua kama mtoto amepatikana tu bila wazazi hatujuhi kama ni ….(Inaudible) wala, pia hatutajua umri ni wake. Lakini tunasema akionekana kama ana miaka nane na akajaribu kufanyiwa upepelezi na hawezi kujulikana ni wa wapi tutamchukua kama mtoto wa nani, wa Kenya na tutampa uraia wetu. Na wengine wanatuuliza kwa nini Tume imefikiria miaka nane kwa nini si miaka tisa. Kusema miaka nane si mtoto wa miaka nane kurudi nyuma, tulisema mtoto wa miaka kumi na mbili anajijua anaweza kujua kwao ni wapi, anaweza kuzungumza lugha na anaweza kujieleza. Tena tukasema, nafasi nyingine mtaona kuwa tumesema mtoto wa Kenya ni lazima awe shuleni kwa hivyo tunataka kumchukulia mtoto mwenye tayari tunaweza kumweka kwenye shule.

Tumesema pia watu wanaweza kuwa na uraia mara mbili hiyo yenye iliandikiwa mara mbili ni dual citizenship, kwa hivyo unaweza kuwa na uraia wa nchi fulani mbili. Kwa hivyo tumefikiria hayo. Tulipoenda kwenye mipakani yetu tuliwapata Wakenya wengi wanye kuishi upande moja wa mpaka na upande mwingine kama Wamaasai walitueleza, sisi wakati wa kiangazi tunapeleka mifugo yetu wapi? Tanzania na hiyo ndio uchumi wetu kwa hivyo tungetaka kuweza bado kuenda Tanzania na kurudi Kenya tusiende bila tashwishi yoyote. Mkisema tukikaa Tanzania tusirudi hapa ama tukikaa Kenya na Tanzania basi mnaua uchumi wetu na tukasikia hiyo ni kweli na ni haki. Pia Wasomali wenye kukaa karibu na Somalia na Ethiopia walitueleza vile vile. Sisi wafugaji wakati tuna kiangazi kwa kila nchi moja tunaenda kwenye nchi nyingine na tukifungiwa huo mpaka basi tuwe na kiangazi Kenya ni lazima sisi tuweze kufanya nini, tutakufa na ya nchi ya Tanzania itafanya nini, itakufa. Kwa hivyo tuangalie kwani hiyo ndio maisha yetu. ***(Child crying in the background).*** Tafadhali mama hata mtoto ana haki zaki katika Katiba yake, lakini hasimkataze mwingine pia kusikia, mtoto una haki ya kuja hapa na kusikiza Katiba yako wewe ndio mwenye utakaa nayo kwa muda mrefu kuliko sisi wengine pengine angetaka kufanyiwa ….

Basi tumakubali hiyo, tumesema mipakani ya….jamii gani pengine tunakaa upande huu wa Kenya na upande huo mwingine.

**Speaker:** Sabaoti.

**Com. Salome Muigai:** Sabaoti wako Uganda na Kenya na nani mwingine?

**Speaker:** Wa Bukusu.

**Com. Salome Muigai:** Wa Bukusu wako upande huu na upande ule mwingine, nani mwingine. Wateso pia.

**Speaker:** Wajaluo.

**Com. Salome Muigai:** Wajaluo na nani mwingine, Samia, Kuria. Pokot wako upande gani nyingine, basi ndio yenye ilitufanya kuweka hiyo habari ya kuwa mtu anaweza kuwa raia wa nchi mbili.

Tulizungumza pia vile mtu anaweza kuanzisha uraia na tukazungumza pia vile uraia wa mzazi mwenye amekufa kabla mtoto kuzaliwa, huyu mtoto tutafanya nini naye. Tumekubali huyo mtoto atapata uraia wa vile amepata kama mzazi hangekufa, kwa hivyo kama alikuwa mzazi Kenya na angerithisha mtoto wake huyo uraia bado utamridhisha huo uraia hata baada ya mzazi kufanya nini, kufa ama kuaga dunia. Tumezungumzia habari ya makao, watu gani wanaweza kuja na kukaa kwenye nchi hii yetu, tumeeleza pia uwezo wa Bunge kwa kikazi ya kiraia na tumeeleza habari ya almashauri. Tutaanzisha almashauri ya usajili wa raia yani Tume ya kusajili uraia. Kitu kingine kimoja kimetofautiana na Katiba iliyoko wakati huu, katika hiyo Katiba mwanamme Mkenya akioa bibi mgeni yaani akioa Mrwanda, akioa Mzungu, akioa Muhindi anaweza kumridhisha uraia, lakini Katiba iliyoko sasa inasema mwanamke Mkenya akiolewa na mgeni hawezi kumridhisha bwana wake uraia. Sasa hiyo akina mama wengi na pia wanawake wengi walitueleza hiyo sio usawa, tumesema Wakenya wote wana usawa katika Katiba. Tukisema wana usawa katika Katiba hatuwezi kuendelea tena kuwapa usawa na mkono mmoja na kuondoa na mkono mwingine kwa hivyo mtu yoyote mwenye kuoa ama kuolewa na Mkenya anaweza baaba ya miaka mitatu kuweka ombi na atafanywa nini, Mkenya. Zaidi na hayo watoto wenye wanatoka kwenye hiyo ndoa ikiwa mzazi mmoja ni Mkenya watoto wana haki ya kuwa nini, Wakenya mnaelewa hiyo.

Sura ya tano inaeleza juu ya sheria ya haki, inazungumzia habari ya haki za kimsingi na uhuru, inazungumzia pia ni wajibu wa serikali kuendeleza haki na uhuru. Inazungumzia pia mipaka ya haki yaani haki ni kitu gani. Una haki zipi? Tumesema kuwa una haki tofauti, una haki za kuishi, you have a right to life, haki ya uai na kwa ajili ya hii haki pia tumeondoa adhabu ya kifo tumesema huwezi kumwambia mtu ana haki ya kuishi na hiyo haki hakupatiwa na mtu amepatiwa na Mungu kwa ajili ni mwanadamu. Una haki zenye hukupatiwa na mtu kwa hivyo mtu hawezi kukupokonya nini, hizo haki na haki moja ni ya kuishi ama haki ya uai na kwa ajili ya hiyo nimesema kuwa tumependekeza tuondoe adhabu ya kifo.

Tumezungumzia pia haki ya usawa ya kuwa kila Mkenya ana usawa mbele ya Katiba ama mbele ya sheria. Wakati mwingine tunaambiwa kwenye nchi zingine kuwa ukiwa mshaidi wewe mwanamme na kuwe na mwingine mwanamke mwenye ana ujuzi wa kupinga lazima kuletwe mashaidi wangapi, wawili ndio akanushe ushaidi wa mwanamme huyo. Mmesikia mambo kama hayo, lakini Wakenya tunasema tuna usawa mbele ya Katiba na mbele ya sheria. Inazungumzia pia uhuru kutokana na ubaguzi, tunasema una uhuru kutogabuliwa, usibaguliwa kwa ajili wewe ni kabila fulani, wewe ni wa dini fulani, wewe ni mama unabaguliwa kwani wewe ni mjamzito ama mambo kama hayo. Kwa hivyo Katiba inasema kuwa una uhuru wa kufanya nini, una uhuru wa kufanya nini?

**Audience:** Wa kutobaguliwa.

**Com. Salome Muigai:** Wa kutobaguliwa, una uhuru usibaguliwa kwa hali yoyote ile. Tunazungumzia pia haki za wanawake. Kuna kipengele kizito hapo kweli kiinazungumzia haki za wanawake. Kuna pia haki za wazee katika jamii, tumesema wazee wetu wameitumikia hii taifa kwa muda mrefu ndio imefika pahali iko kwa hivyo wana haki zao. Haki moja ni kuwa ni jukumu ya kila mzee kujipanga mali yake ili atakapokuwa mzee aweze kujisitiri lakini ikiwa mbali na hiyo mpangilio ana shida ya kukosa mahali ya kuishi, ana shida ya chakula serikali inawajibu wa kufanya nini, kumlinda. Kwa hivyo hiyo ni moja ya haki zenye ziko zingine mtazisoma.

Tumesema pia kuna haki za watoto, watoto ana haki ya kusikilizwa, mtoto ana haki ya kuwa na jina, mtoto ana haki ya kulindwa na kutunzwa na nani? Baba na mama, wazazi ni nani? Wakati mwingine tunasahau wazazi ni nani, wazazi ni nani?

**Audience:** Baba na mama.

**Com. Salome Muigai:** Mama anaweza kuwa mzazi akiwa peke yake? Baba anaweza kuwa mzazi akiwa peke yake?

**Audience:** La.

**Com. Salome Muigai:** Na kwa nini watu wengi hawana wazazi wawili, hawatunzwi, hawalindwi. Hii Katiba inasema baba na mamam wanamlinda mtoto na kumsimamia. Anasimamiwa na nini, na Katiba na hii Katiba itawasurutisha wazazi kumtunza, kumhudumia na kumlinda nani? Mtoto. Kwa ajili tulisema watoto wetu ndio nini, watoto ndio usoni wetu. Unaweza kuwa mkulima ukiwa wewe hupandi? Ukipanda inatosha? Unahitaji ufanye nini? Watu wengi hata hawa…. Ukipanda ni lazima ufanye nini kabla ya kuvuna?

**Audience:** …(Inaudible)

**Com. Salome Muigai:** Ukikataa kuvuna sisi tutakuja kukuvunia lakini kabla ya kufika pahali pa kuvuna ni lazima ufanye nini?

**Audience:** Upalilie.

**Com. Salome Muigai:** Ni lazima ipaliliwe na lazima ifanyiwe nini tena? Itunzwe wakati kuna haja basi na watoto wetu ni hali kadhalika, lazima wakizaliwa wafanywe nini, watunzwe na tumesema kwa kirefu bahari ya haki za watoto. Tafadhali zitazame na usome nyumbani.

Tumezungumzia pia habari ya haki za familia, tumesema Katiba yetu ni lazima ilinde, familia kwa njia tofauti, yenye pia mtasoma. Tumesema pia Katiba yetu iko na haki ya nani, watu wenye ulemavu. Tumesema watu wenye ulemavu wana haki, wana haki ya kuweza kuingia kwenye hili jumba kama mtu mwingine yoyote si hii ni jumba la nini, this is a public building. Jumba la nini?

**Audience:** La uma.

**Com. Salome Muigai:** La uma, basi kila mtu ana haki ya kuweza kuingia kwenye hiki chumba. Sasa tumesema ni lazima tuangalie mijengo yetu kila pahali ituwezeshe kila mtu kuweza kufanya nini? Kuingia na kutoka. Tumezungumzia mambo mengi, tumezungumzia habari ya elimu kuwa vituo vyetu vya elimu vyovyote lazima ziwezeshe watoto wetu wenye ulemavu kuweza kuingia na kusoma kule na kutoka na kuhitimu. Tumezungumza pia habari ya heshima za binadamu, you must be respected na hii Katiba mpya inataka kulinda heshima za nani, za binadamu. Binadamu ni nani? Mama binadamu ni nani?

**Speaker:** Ni mimi.

**Com. Salome Muigai:** Ni wewe na binadamu ni nani, ni mimi na mwingine. Basi tunazungumzia habari ya heshima za binadamu, tunazungumzia pia uhuru na usalama kwa mtu. Usiomfikia wewe mwenye ndio uleta usalama, mambo mengi yote itafanyika? La, ukiwa hutapata security hatutaweza kuyatunza yale mengine kwa hivyo hii Katiba imeeleza habari ya usalama wa mtu. Hii Katiba pia imesema hakuna mwananchi wa Kenya atakayewekwa kwenye nini, kwenye utumwa, kwenye sulubu ama kwenye chokoa. Hiyo mambo imekuwa mengi zaidi saa ingine Kiswahili kinakuwa kigumu kuliko Kiingereza, si hivyo. Tunasema hakuna Mkenya mwenye atawekwa kwenye utumwa, hiyo tunaelewa si hivyo? Pia hakuna mwenye atafanywa kufanya kazi ya bure kwani hiyo pia ni utumwa na tumesema kuwa hakuna mtu atakayelazimishwa kufanya kazi isipokuwa ukivunja sheria basi na wewe unakatisha uhuru wako wa kikazi. Uhuru wako ni wakati wenye unafuata Katiba na unafuata sheria, kuvunja sheria pia kunakatisha hiyo uhuru na hizo haki.

Tumesema kuwa kila mtu ana haki ya faraga, privacy yaani nyumba yako ni yako na hakuna mtu mwenye anahaki ya kuingilia tu ovyo ovyo. Nikiwa mimi ni mwanaserikali na ninataka kuingia nitahitaji kufuata masharti fulani ndio tuweze kuingilia faraga yako.

Uhuru wa dini, imani na maoni pia umelindwa. Watu wengi wametuuliza na walitueleza kuwa kumesemwa uhuru wa dini ni lazima iwe ni dini ya kumwabudu Mungu na sio nani, shetani. Lakini nayo sheria inakikomo chake ukisema ni lazima watu waabudu Mungu ni lazima utafsiri Mungu ni nani na ni nini na shetani ni nani na ni nini? Sisi tulipofikiria hiyo habari kwa muda karibu masaa matatu manne na tukaenda kulala tukaamkia tena tulikuwa na tashwishi kubwa ya kujaribu kutafsiri Mungu ni nani na shetani ni nani kesheria sio kiimani. Kiimani tunajua lote lakini mtu akikuambia u-prove in a court of law huyu ni Mungu na huyu ni shetani ilitupa tashwishi kubwa kwa hivyo sisi tuliachilia hapo tukasema mtu ana uhuru wa kuabudu. Lakini tukasema pia tutahimiza Bunge iunde sheria zingine zenye kusema huwezi kutoa fakara ya watu, huwezi kufanya mambo mengine yenye

inahusiana na huo kuabudu hawa watu wengine lakini kwa hii inalengo iwapo katika Katiba hatukuweza kuenda zaidi ya hapo. Ningetaka pia kukueleza kuwa Katiba ni mwelekeo, is broad principles. Katiba haiwezi kuwa na kila jambo, Katiba inakuwa na broad principles. For example, nikisema mimi Katiba imenilinda nisibaguliwe basi Katiba haiwezi sema usibaguliwe kwa uchaguzi, usibaguliwe kwa chakula kwa ajili ikisema hivyo zile vitu vyote venye haijasema unaweza kubaguliwa kwa vitu hivyo. Mnaelewa? Kwa hivyo Katiba inapeana principles halafu hizo mambo mengine zinatekelezwa kwa sheria na sera, policy.

Halafu pia tumezungumzia habari ya uhuru wa kutoa maoni, wewe ukiwa na maoni yako Katiba inakusimamia kutoa hiyo, maoni yako. Inasema tena unaweza hata kuchapisha hayo maoni yako mradi tu hayo maoni yako isichochee chuki kati ya watu. Ikiwa hiyo maoni yako inasema watu wote warembo hatuwataki kwa ajili hawa ni nini na nini basi hiyo uhuru huo wako umefanya nini, umeikeuke kwani uhuru wake na haki zako lazima iishie pahali uhuru na haki za mwingine inaanza. Huwezi kuwa na uhuru isiyo na kikomo lazima uhuru wako ukomee pale haki za mtu mwingine, inaanza.

Tuko pia na uhuru wa kufikia habari, habari zenye ulitaka news or information una uhuru wa kutaka wizara yote ya serikali ikupe habari zenye ungetaka. Pia tuna uhuru wa kushirikiana yaani uhuru wa kuja pamoja, uhuru wa kukutana mahali na kuchochea mgomo kwa hivyo kuna uhuru wa kugoma na uhuru wa malalamiko. Hii Katiba inasimamia kuwa mtu anaweza kugoma, unaweza kulalamika, unaweza kuandamana, unaweza kukutana bali tu ufanye mambo yako kwa nini, kwa usalama, usitatize usalama.
Pia umepatiwa haki za kisiasa, una haki za kisiasa, una uhuru wa kuenda utakako na kukaa utakako kwenye hii Jamhurii ya Kenya wewe ukiwa ni Mkenya unaweza kuenda pahali popote pale unaweza kukaa pahali popote pale. Kuna haki ya wakimbizi na hifadhi yaani watu wengine wakikimbilia kwenye hii Jamhurii yetu tutawapa hifadhi. The right of refugees and asylum seekers. Kuna uhuru na haki ya kuwa na mali, hii ina maana gani? Ina maana kuwa ukitafuta mali yako na ukaipata una uhuru wa kuwa nayo na mtu mwengine asiingilie lakini mradi tu huo umeipata kwa njia gani, ya halali. Kuna haki ya uhusiano kikazi yaani labour what? Can you read it louder? Tuna waalimu kwenye hiki chumba na wasomi? Bwana Jumbe alituambia yeye ni mwalimu kwa nini hatusikii sauti ukitusaidia na Kiswahili na Kiingereza. You have a right of what?

**Audience:** Labour relations.

**Com. Salome Muigai:** Labour relations. Una haki ya afya na una haki ya nini?

**Audience:** Ya elimu.

**Com. Salome Muigai:** Ya elimu, ya makao na nyumba, una uhuru wa chakula, maji safi. Una uhuru wa usafi pia, una haki ya usafi, tuna haki za mazingira na kila mtu pia anajukumu ya kulinda mazingira. Tuna uhuru wa lugha na kitamaduni, yaani una uhuru wa kutumia lugha yako. Tuna uhuru wa haki za wateja, mimi kama mnunuaji ama consumer nina haki zangu na inalindwa na hii Katiba. Una haki za utawala wa haki, you have a right to what?

**Audience:** Fair administration.

**Com. Salome Muigai:** Fair administration, ukienda kwenye ofisi ya headmaster wa shule pale watoto wako wanasoma una haki ya kuhudumiwa. It is your right kwa ofisi yoyote ya serikali kwani ofisi hizi zote zinatekelezwa kwa pesa zinazotoka wapi? Zinatoka kwa nani?

**Audience:** Kwa wananchi.

**Com. Salome Muigai:** Zinatoka kwangu na kwako kwa hivyo tunahaki ya huduma bora. Una haki ya kutofuata maagizo yasio halali, you have a right to do what or not to do what? Hii ilitokea sana kwa ajili ya janga iliyoipata Rwanda, watu wenye waliuwa wakiulizwa wanasema mimi nilikuwa nafuata nini, nilikuwa natekeleza nini? Amri, basi sasa hii Katiba inasema ukiambiwa uua mtu mwingine huendi tu kuua bila kuuliza swali na ukiua ukifikishwa kotini hutajitetea ukisema ulifuata amri. Una haki ya kufika mahakama, unahaki ya kuweza kufikia mahakama kila mmoja. Sisi wenye kutumia magulududumu hata kufika huku kwenyewe inakuwa shida.

**(Interjection)**

**Com. Salome Muigai:** Telephone interruption. Ningetaka kuuliza watu wote wazime mobile na mimi hata sikufanya hivyo lakini kwa ajili ilitoka ofisini juu ya mambo fulani ndio nimechukua hivyo nimewacha na sitachua nyingine na ningetaka kuomba wengine mzime simu zenu.

Haki ya kufikia mahakama kwa hivyo ikifikia mahakama physically lakini pia unaweza kutizwa ukienda mahakamani. Wenzetu wenye hawatumii masikio wanaona kwa ishara wanakuwa na shida kubwa sana kusikia wakifikia mahakama, ingawa umeshafika kule. Sasa tunasema kila mtu Kikatiba ana haki ya kufikia mahakamani. Kuna watu za watu wanaotiwa nguvuni, ukitiwa nguvuni una haki zako. Watu wengi walituambia wakienda mahakama hata kabla hawajafikishwa kwenye mahakama umechapwa ama umefanyiwa madhara, umeumizwa. Tunasema kuwa kwenye hii Katiba mpya mwenye amewekwa nguvuni ana nini ana haki zake na utaziona kwa wingi kwenye utaratibu wa hicho kituo uone unasema nini.

Kuna haki ya waliowekwa kizuizini pia wanahaki zao, wenye kufanyiwa mashtaka ya haki pia wanahaki zao na una haki ya kufanyiwa mashtaka ya haki sio kuingiziwa kwenye mambo yenye ujafanya unapelekwa mashtakani. Watu wengi walituambia tulipokuwa tukipata maoni kuwa wakati mwingine ukipelekwa polisi inakubali hatia isiyo yako ndio uwekwe kwenye rumandi siku mbili mwezi mbili au miezi tatu. Basi walioshtakiwa wanaenda kwenye koti na kukubali hatia zenye hawako nazo ndio waweze kutoka. Tunasema sasa una haki ya kushtakiwa kihaki, ile isiyo ya haki usifanye nini? Usishtakiwe kwa mambo isiyo ya haki.

Wakati ya hali ya hatari mara nyingi haki nyingi zinaondolewa kwa muda kwa hivyo tumezungumzia kuwa, kukiwa na hali ya hatari kuna masharti fulani yenye itatakikana kuwekwa. Kwanza kuzizambazwa hali ya hatari kufikia muda fulani ni lazima Bunge liwe limeuhusishwa kujua hali hii ya hatari itaendelea kwa muda gani na ni sababu gani. Halafu tujue haki zetu zimehadirishwa kwa muda gani, kuna haki ya kujua hivyo.

Mwishoni tunaweka Tume ya haki za binadamu na haki za utawala ama kuunga mkono haki za binadamu hizo tumeweka pamoja. Ya kwanza ilikuwa tutaweka Tume yenye kusikiliza malalamishi ya watu ikiwa haki za binadamu zimekiuwa na pia tunao kuifikisa mahakama kwenye hii Katiba kuwekea maanani na kulinda hazi za binadamu. Mamlaka ya mahakama kuunga mkoni, hiyo ime….(Inaudible) Halafu mwisho wa hiyo sura kuna ufafanuzi, niliwaambia kwa kila sura ya sheria lazima ufafanue kuwa ukisema haki una maana gani, ukisema neno hili una maana gani. Kwa hivyo hapo mwisho ya kila sura utapata ufafanuzi. Imeendelea kwa kila kiwango ya sura ya haki au sheria za haki kwa sababu malalamishi nyingi yenye tulipata kwa wananchi kote nchini ilikuwa juu ya kukiukwa kwa haki zao lakini hizi sura zingine hatujaendelea neno kwa neno, tutaenda kwa utaratibu kwa upesi kidogo.

Sura ya tisa ni uwakilishaji wa watu na tumeigawanya kwenye sehemu tofauti. Sehemu ya kwanza ni taratibu wa upigaji wa kura, tumeseka kuna kanuni za kura na kuna uchaguzi, tuna haki ya kupiga kura na tuna sifa za mtu kusajiliwa na kuna kutostahili kusajiliwa. Kitu gani unahitaji kufanyi ili usajilishwe kama kupiga kura, kitu gani unaweza kufanya kujistahili kupiga nini, kura ama kusajiliwa kupiga kura. Kinaeleza vile utakapopiga kura na pia inazungumzia juu ya wagombeaji bila kupingwa. Ningetaka kusema mambo mawili juu ya kura, upigaji wa kura. Tofauti zipi zilizoko kati ya Katiba iliyoko sasa na Katiba hili, mapendekezo ya hii Katiba mpya. Katiba Katiba iliyoko sasa tunapiga kura na mtu mwenye kupata kura mingi zaidi ndio mwenye amefanya nini, ameshinda na watu wangapi wanashinda? Mtu mmoja, sasa tumependekeza kuwa tukienda kupiga kura watu watapiga kura mara mbili, utapimpia Mjumbe wako na utapigia chama. Unaweza kumpigia Mjumbe mwenye amesimama na hicho chama na ndio mwenye unampigia kura, unaweza pia kumpigia Mjumbe mwenye anasimama na chama kimoja na upigie chama kingine tofauti. Tofauti gani tunasema hivi, wacha niwapeleke nyuma kidogo pia. Tulipokuwa tunapata habari kutoka kwenu watu wengi walitueleza watu wenye watakaa kwenye kikao penye watu wengi kama Uashi Ngishu, katika Ugunja, Murang’a na Westlands na Vihiga walitueleza kuwa kikao cha Bunge tukitaka kufanya mipaka ya kikao cha Bunge tuangalie nini, tufanye nini?

**Audience:** Wingi wa watu.

**Com. Salome Muigai:** Wingi wa watu na kila pahali penye watu wengi walituambia vile lakini tusiangalie nini, ukubwa wa eneo. Halafu wakatuambia sisi hatutaki pia watu wanawakilishwa vipi na wanawakilishwa lipi, umoja ni kuwakilisha watu. Tulipoenda North Easten, Mandera, Wajia na wapi tena, Garisa pia pahali pengine ya Rift Valley kama Kajiado, Trans Mara hata hapa Marakwet. Tukaambiwa nyinyi mkianza kufikiria habari ya vikao vya Bunge ni lazima mfikirie eneo, kwani mahali ya wengine iko mbali sana mtu anaweza kuenda mile mia tano bado hajafika kwenye mji mkuu pahali watawala wako, kwa hivyo

tungetaka muangalie habari ya maeneo ndio tuweze pia sisi tumefaidika. Mkiangalia wingi wa watu, muangalie nini, eneo. Sasa sisi kama Tume wenye walituambia tuangalia eneo ni wa kutoka wapi, Kenya. Wenye walituambia tuangalie tuangalie wingi wa watu ni kutoka wapi, Kenya. Basi baada ya kujadiliana kwa muda mrefu tukafikiria tutaleta mchanganyiko ya haya mambo mawili kwa hivyo kwa uchaguzi tutaleta mambo mawili. Ikiwa mna eneo kubwa au ndogo bado nyinyi mtapigiwa kura sehemu hiyo mtakaa na mtapata Mjumbe wenu lakini pia mtapigia chama. Kwa hivyo watu wenye ni wengi kama Uasin Gishu na wapigie chama kimoja watakuwa wakipatiwa vitu vya siada, sio tu ni Mjumbe mmoja ndio walipata lakini ni chama kipi lilicho kubwa katika kikao cha Bunge cha Eldoret ya Mashariki?

**Audience:** KANU.

**Com. Salome Muigai:** KANU na gani ingine, ni KANU peke yake. Haya, basi tuseme ni KANU peke yake nyinyi mko watu wengi mpige kura zenu mumpigie Mjumbe wenu na pia mupigie KANU, hii kura ya KANU zitahesabiwa ni ngapi na kulingana na wingi wa kura zao watapatiwa viti vingine katika Bunge vya ziada. Je hivi viti vitasaidia je? Hivi vitu ndivyo venye vitasaidia kuleta wenye hawawezi kuenda kuleta mtu kwa kura. Kwa mfano, ikiwa nyinyi mnakaa Moi Ben, that is Eldoret East isn't East? Pia ni Eldoret ya Mashariki na Moi Ben kuna kabila ngapi, nani anatoka Moi Ben hapa? Umetoka Moi Ben, Moi Ben kuna makabila gani? Kuna Wakalenji, Wakikuyu, kuna Waria pia. Mjumbe wa Eldoret East ni nani?

**Audience:** Tarar.

**Com. Salome Muigai:** Tarar, ametoka kwa jamii gani? Kalenjin kwa hivyo kama KANU ikimuigiza huyu Mweshimiwa Tarar na wakapata viti vingine vitatu ama vine hiyo ni nafasi ya kuwaleta watu wengi zaidi kwenye uongozi. Wanaweza kusema kitu moja tutapatia Waluhya, ingine tutapatia akina mama na chengine kama ni nne tunaweza pia kumpatia mtu mwenye ulemavu ndio kila mtu auzishwe kwenye utawala. Lakini tukisema tu watu wanataka kuenda Bunge kwa ajili ya kuchaguliwa peke yake kuna watu wenye hawataweza kuakilishwa miaka yao yote na kila Mkenya kama ni demokrasia, demokrasia inasema kila mtu ana haki ya kuwakilishwa na watu wengi pia wanasema naye asiyekuwa na lake halipo. Kwa hivyo hii mjadala unapendekeza kuhuzisha watu wengi zaidi kwenye Bunge ama kwenye utawala ili ukienda Bunge ya Kenya uweze kufikiria kama unakuja kutembea pahali pengine aah, kumbe Kenya kuna makabila na mna watu ili unahesabu kabila zenye ziko Bunge unahesabu akina mama, unahesabu vijana, unahesabu watu wenye ulemavu na unaona sura ya Kenya katika Bunge ama katika utawala wowote. Kwa hivyo ndio tunasema hii pendekezo inataka kubadilisha nchi yetu na tuongezee ili tuweze kuwakilisha watu wengine ndio vile vitu vya ziada mnasikia tisaini.

Kila chama chenye kupigiwa kura nyingi vitakuwa na viti hivi na vitaelekezwa katika Katiba watu gani wataweza kupatiwa hivyo viti. Tumesema pia hizo viti ndio tutaenda kuwapatia wataalam, tunaenda kusema ijapo watu wa Uasin Gishu uchumi wetu ni wa nini, ni wa kilimo kwa hivyo zaidi wa mweshimiwa wenu mngetaka kuwa na mtaalam wa kilimo kwenye Bunge ndio awe akitetea shida za ukulima. Sasa hiyo ndio nafasi yenye inatolewa ama pia tunaweza kuwa na mzee, ni mzee wa miaka

sabini ama sabini na tano yeye hawezi campaign lakini kila pahali tukiwa na utatanishi kila mtu atajua mzee fulani akija hapa tutaweza kufanya nini? Tutaweza kutumisha hili jambo. Basi hii ni nafasi ya watu wa Eldore ya Mashariki kusema mzee fulani ingawa hawezi kazi ya campaign ni mwakilishi mwema kwetu basi apatiwa moja ya hizo viti. Hiyo ndio tofauti moja ya upigaji wa kura yenye humo wakati huu na ile yenye tunapendekeza.

Jambo la pili ni kuhusu kupiga kura, zamani ilikuwa mtu kama hana mtu wa kukulinda basi hakuna haja ya kupiga kura lakini wakati huu tutahitaji kupiga kura ndio pia tufaidike kwa kura zetu na pia tuende tukapige kura ndio tupigie chama chenye tunataka kupigia. Sasa kama hatujapingwa ni lazima tukipiga kura watu wako wajitokeze na wafanye nini, wapige kura. Hayo ndio mambo mawili ninazungumzia kwenye hiyo sehemu.

Sehemu ya pili ni juu ya Tume ya uchaguzi, utaundwa Tume ya uchaguzi, tumeeleza majukumu ya hiyo tume, tumezungumzia juu ya wafanyikazi wa hiyo Tume na mipaka ya maeneo ya Bunge. Tumesema kila miaka kumi tukifanya census, tukihesabu watu na tume ya uchaguzi itakuwa na jukumu ya kuangalia mipaka ya nini, ya maeneo ya Bunge. Pia hili Tume mpya yenye tunapendekeza tumepungua watu wenye watakuwa kwenye hiyo Tume, tumesema itakuwa na watu wasiopungua nane na wasiozidi kumi ili iwe Tume ndogo yenye inaweza kufanya kazi nyingi, ikihitaji watu wengine tutaweka wafanyikazi wenye wataajiriwa kwa ajili ya kuhitimu kwao. Pia tumeipa hii Tume ya .. Tume ya nini tunazungumzia?

**Audience:** Uchaguzi.

**Com. Salome Muigai:** Ya uchaguzi, nikisema haya ni kuangalia kama mnasikiliza nangoja nisike kama mtanipe neno lenye linatakikana. Kwa hivyo pia tumesema hii Tume ya uchaguzi tutaipa kazi ingine moja ndio itasajiri vyama vya kisiasa. Kwa sababu gani, hawa wanapokwenda kusimamia uchaguzi ndio wanaona chama gani inafujo, chama gani kinaweka maanani ambayo pia inafanya uchaguzi wenye amani na wenye nidhamu. Kwa hivyo wenyewe wawe ndio wenye kusajirisha nini, vyama vya kisiasa ili vyama vya kisiasa vijue huyu ni msajiri wetu na ndio mwenye atakuja mashinani kuona tabia yetu wakati wa kura ili tuanzishe mfumo wa kura lisivyo, na fujo.

Sehemu ya tatu inaeleza juu ya vyama vya siasa, tumeeleza kuwa una haki ya kuunda chama wakati yoyote. Tumeeleza wajibu na majukumu ya vyama vya siasa, tumezungumzia juu ya usajili wa vyama vya siasa nimewaeleza tayari. Tumeeleza sifa za chama kusajiriwa yaani qualifications ndio chama kisajiliwe na sifa na haki ya ushirika yaani wana haki ya kufanya nini, they have a right to do what in number 91.

**Speaker:** To be a body cooperate.

**Com. Salome Muigai:** To be a body cooperate, wana haki ya ushirika, ni chama chenye kitaweza kupelekwa mahakamani na inaweza pia kukupeleka mahakamani. Na pia tumesema vile usajiri inaweza kuvunjwa, chama kitafanya nini ili hata tukiwa

tulikuwa tumesajiriwa kifutwe.

Imezungumzia juu ya hazina ama mifuko wa vyama vya siasa, tumesema kuwa vyama vya siasa ni lazima vipatiwa pesa za uma hiyo ndio mapendekezo yetu hata magari kwa sababu huu uwanja yenye viama vya kisiasa vinavyochezea kandanda hautoshani kamwe. Unaona pahali pengine unadunda kabisa ili mtu akikupigia mpira upande huu unaenda moja kwa moja mpaka goal ya nani, ya yule mwengine. Kwa hivyo tumesema vyama vitapewa peza za uma lakini kuna masharti yenye hivi vyama lazima zitosheleze. Kwanza ni lazima kiwe chama cha taifa sio cha kikabila, pia lazima hicho chama kiwe kwenye uchaguzi kimepigiwa theluthi kwa mia, three percent of the national vote. Kwa hivyo ingawa tuna vyama vingapi sasa?

**Audience:** Ingawa tuna vyama zaidi ya hamsini tukiweka kwenye kichungi tukizichunga kwa hii masharti nyingi zitatoboa? La lakini tunasema kama uma ndio wenye wana hifadhi hivi vyama lazima viwekewe masharti fulani ya kufuata na ya kutimiza. Tunasema pia habari asili ya mifugo itatoka wapi, ma-boom ya mifuko, fedha nyingine za vyama vya kisiasa yaani kama mtu anataka kuanzisha chama kutakuwa na amri yenye pesa zenye unawaza kuchangia uwezi kuchangia zaidi ya hivyo. Kwanza hatutaki vyama vikuwe maziwa ya kuuza na kufanya nini, ku nunua. Chama ni cha wananchi na hatuwezi kuwa tuna mtu mmoja kuweza kuunza na mwingine kuweza kununua. Tunazungumzia habari ya usimamizi wa vyama vya kisiasa na nidhamu ya vyama na pia tunazungumzia matumizi dhidi ya matumizi ya mali ya uma. Tumesema kuwa chama hakikubalishwi kutumia rasilimali ya uma kufanya campaign, lazima chama ikishapatiwi pesa zake kitumie hiyo ili vyama vyote viwe na usawa ya kufanya nini?

**Audience:** Ya kufanya campaign.

**Com. Salome Muigai:** Zinafanya campaign ndio zifanye nini? Zinashindana si hivyo, vyama vinashindana kwa hivyo tunataka nafasi sawa ya kushindana. Tumezungumzia juu ya kizuizi dhidi ya nyadhifa katika vyama vya kisiasa, kitu gani kinaweza kukataza kuwa kuna wadhifa chama.

Sasa tuendelee kwa kura ya saba hiyo ilikuwa sura ya sita. Kura ya saba inazungumzia juu ya sheria. Sheria ya kwanza ni ya Bunge. Tunazungumzia vile Bunge itaundwa, tunazungumzia pia wajibu wa Bunge na tunazungumzia kuhidhinishwa kwa uteuzi wa Bunge na tunazungumzia idhini ya matumizi ya fedha na Bunge.

Sehemu ya pili tumezungumzia muunda na uwanachama wa Bunge hapo kuna tofauti mbili zenye ningetaka kuchangia. Moja ni kwamba tutakua na Bunge lenye vikao viwili, ya kwanza ni kikao cha watu wenye tunachagua moja kwa moja. Kikao cha pili kitakuwa na watu watakaochaguliwa kwa kila wilaya, kwa hivyo itakuwa kuja kuwa na watu wangapi? Sabini hivi na tumesema hii pia katika kila kikao cha Bunge lazima theluthi ikuwe nani, wanaweke. Kwa hivyo tumetoa viti vingine thelathini zenye kila wilaya, kila mkoa itatuletea akina mama wanne, ya Nairobi itatuletea wawili ndio wawe thelathini wakae kwenye kikao cha baraza la taifa. The National Council. Kwa hivyo tunasema tunataka watengewe viti fulani, watu wengi wamelalamika tumepata kila pahali tukienda wanalalamika, mmesema sisi tuko sawa halafu unarudi kupata akina mama

wanategewe viti tofauti, sasa hiyo usawa uko wapi?

Basi tunasema usawa sio kusema tunafafana, ingawa tuko sawa tunatofauti na kwa muda mrefu akina mama hawakuwasilishwa ama hawakuletwa kwenye utawala kwa hivyo tukisema ingawa kwa mfano wenye waliniona nikija mliona mimi nina ulemavu si hivyo? Nikisema kutoka leo kila mtu atoke kwa hiki kikau kila mtu aende zake tuanze kuandamana, kitambo mtu wa kwanza afike sokoni mimi nitakuwa bado niko wapi? Kwa gate, haya mtu akipiga firimbi aseme kutoka sasa firimbi stop where you are kutoka sasa tuko sawa kila mtu atatembea kwa mwendo wa sawa. Je, hata ukianza kutembea kama mimi hapa na mimi siwezi kutembea kama nyinyi kuna wakati yenye nitawafikia? La. Kwa hivyo tukiomba mtu mwenye gari atuambie wewe kwanza chukua Madam Commissioner mfikishe pale sokoni ndio afikie watu wale wengine, si ndio. Bila hivyo nitawafikia? La. Kwa hivyo ndio tunasema akina mama wamebaki muda mrefu, walemavu wamebaki muda mrefu. watu wenye jamii ndogo ndogo wamebaki nyuma muda mrefu kwa hivyo tuwapige jecik kidogo wafike ingawa pale mbele kwa muda fulani, siku ile mambo itakuwa sawa sawa tutaondoa. Ukiweka gari nje kitunaweka kwa miaka yote, ni lazima ukimaliza mambo yako utoe ndio tuendelee. Ndio kwa sababu tunasema akina mama, watu wenye ulamavu, vijana na watu wenye hawakufika mbeleni kwenye utawala wapatiwe nafasi kidogo ndio waweze ingawaje kufikia wale wengine.

Sasa nimezungumzia habari ya hali ya Bunge, itakuwa na vikao viwili na sasa ningetaka kuangalia sehemu ya tatu na hiyo ni maafisa.

**(Interjection)**

**Speaker:** Je madam.

**Com. Salome Muigai:** Yes.

**Speaker:** Maswali ni wakati huu ama tutafanyaje?

**Com. Salome Muigai:** Wakati nitakapomaliza wewe weka swali lako chini. Mnakumbuka siku ya maoni nyinyi mlijieleza na sisi tumenyamaza, tukauliza swali wakati wa mwisho sasa ni mpira umefanya nini, umegeuka sasa wakati huu na mimi nawaeleza nyinyi fikirieni swali mlilonalo mwishoni nitawapa nafasi na nyinyi mfanye nini, muulize swali lenu.

Sasa ndio sehemu ya tatu juu ya sheria pia ni maafisa wa wasimamizi na watenda kazi nyingine, hiyo ni habari ya baraza katika hii, itasamiwa na nini, itafanya kazi gani, baraza hilo lingine na wasimamizi ni nani na nani wa baraza la wabunge na kushugulikia kazi za Bunge na kiongozi wa chama cha waliowachache na vitu kama hivyo. Kwa hivyo tafadhali pata nafasi uyasome hayo uelewe.

Sehemu ya nne ni juu ya sheria na utaratibu wa Bunge, wengi wenu walituambia kuwa Bunge ni lazima ipatiwe uhuru wa

kufanya mipango yake yenyewe, si ndio. Na hiyo taarifa imeeleza habari ya utaratibu ya Bunge, vikao vyake, fedha zake, uwajirishi wa kazi ya watu wenye ufanya Bunge na mambo kama hayo pia hiyo inahitaji kusomwa kwa utaratibu.

Sehemu ya tano ni kikao cha ratiba ya Bunge, kikao cha Bunge kitakuwa lini, kuvunjwa na kuwakilisha Wabunge, hoja ya kutokuwa na imani na mambo mengi kama hayo. Mengine ya ziada ni uhuru wa kuzungumza kwa majadiliano katika Bunge, mnajua kuwa Bunge hukubalishwi kushtakiwa na mtu yoyote kwa mambo uliyozungumza ukiwa kwenye Bunge mnajua hivyo? Kwa hivyo inatakiwa kwenye Katiba hii. Pia uwezo na kabila za kinga ya uma na vile uma ama watu watakaposhirikishwa kwenye kazi za Bunge. Ukisoma mia moja na arubaine na sita utasikia mambo gani Tume imependekeza. Pia tumezungumzia habari ya Tume ya huduma ya Bunge.

Sura ya nane ni mamlaka ya nchi. Rais wa Kenya bado ana mamlaka katika hii Katiba, mamlaka gani? Kutaja tu machache yake, Raisi ndio amri jeshi mkuu, Raisi ndio mwenye atakayechagua watu wote wenye kufanya kazi zote katika nyadhifa zote za serikali ingawa atafanya hivyo akiwasiliana na Bunge lakini mwisho ni yeye mwenye atafanya uamuzi wa mwisho lakini Bunge likishakubali. Tumeweka Tume ya usalama wa nchi na mwenyekiti wake ni Rais wa nchi. Kwa hivyo bado ana kazi nyingi yenye anatakiwa kufanya kwenye hii Katiba mpya. Mnasikia mamlaka ya Rais, majukumu ya Rais wa kitaifa, wajibu wa sheria wa Rais, uamuzi wa Rais, upunguzaji wa uwezo wa Rais, haki ya kupiga kura na wakati wa uchaguzi wa Rais. Jambo moja ningeongeza ni habari ya upigaji kura kwa Rais. Tumesema kuwa Rais atamleta mwenzake mwenye angetaka apigiwe kura naye yaani running mate na hawa wawili watapigiwa kura moja kwa moja na raia na wakipigiwa wawe wawili, yeye anakuwa Rais na mwenzake atakuwa mahakamu wa Rais. Na mahakamu wa Rais tunasema wakati Rais hayuko yeye mahakamu anasimamia mamlaka ya Rais. Kwa hivyo atakuwa amechaguliwa na wananchi moja kwa moja. Basi hiyo sehemu ya pili ina mambo mengi sana kuhusu Rais hata kazi mahakamu wake na jukumu yake yameelezwa kwenye hii sehemu.

Tukiangalia sehemu ya tatu ina habari ya waziri mkuu na baraza la mawaziri. Kuna mambo mengi pia yenye mtasoma pole pole lakini mambo matatu ningetaka kueleza. Kwanza Waziri Mkuu atachaguliwa kutoka Bunge kutoka kwa chama chenye Wabunge wengi zaidi kwenye Bunge, na yeye atachaguliwa na Rais, kwa hivyo bado hiyo pia ni mamlaka ya Rais. Atakuwa na wadogo wake ama makamu wake wawili pia hawa watachaguliwa kutoka Bunge. Mawaziri watachaguliwa kutoka nje ya Bunge, swali lenye linaulizwa na watu wengi ni sababu gani mnataka kutafuta waziri wenye hawajachaguliwa na wananchi. Mambo matatu wananchi walituambia, ya kwanza walisema kuwa wakati Mjumbe wangu anakuwa Waziri sitamwona tena mpaka siku ile Rais atakuja kutembea kwenye kikao chetu cha Bunge kwa hivyo ningetaka Mbunge wangu asiwe Waziri ndio afanye kazi yake ya kuwakilisha mimi. Jambo lingine la pili walisema ni kuwa tunataka mawaziri kuwa kumi na tano kwa sababu wanasema, kila mmoja akichaguliwa kuwa waziri ama mdogo wa waziri anaitwaje? Naibu wa waziri na wakati nyingi sana kwa Bunge kuna kuwa Bunge haina mtu wa kututetea tena. Kwanza Bunge haiwezi kupingana na serikali, waziri na manaibu wake hawawezi kupingana na serikali kwani wako serikalini kwa hivyo nani mwenye anamtetea mimi kama mwananchi wa kawaida? Kwa hivyo Mbunge wangu aachwe afanye kazi ya Ubunge. Neno lingine tuliambiwa na wananchi ni kuwa mara nyingi Wabunge wanakaa tu wakingoja kuchaguliwa waziri? Kwa hivyo Mbunge anaogopa kujitetea kwani yeye anangoja

kuteuliwa afaidike yeye mwenyewe. Kwa hivyo tafadhali Wabunge waachiwe kazi ya nini, ya ubunge.

Pia walitueleza Kenya tuna watu wengi sana wenye wanatafuta kazi wacha mtu mmoja akae na kazi ngapi, moja. Last but not least, walisema tunataka waziri akuwe mtaalam kwa wizara yake, akiwa ni Waziri wa Afya lazima awe nani, daktari. Akiwa ni Waziri wa elimu ni lazima awe mwalimu. Akiwa ni waziri wa mambo ya usalama ni lazime awe askari ama mwenye background ya hiyo kazi. Tukaona ukiwa tunataka wataalam itakuwa shida kusema tuwachague wataalam kutoka Bunge wakati wote kwa hivyo hii Katiba inasema, ukichaguliwa na uwe Mbunge urudi upate kuwa waziri ni lazima u-resign kiti hicho na Waswahili pia wanasema ukitaka viwili?

**Audience:** Utakosa yote.

**Com. Salome Muigai:** Hiyo sio mimi nilisema hiyo ni Waswahili na mimi sio Mswahili, kwa hivyo watu wengi wenye walituuliza kwa nini mnasema waziri wasitoke Bunge, sasa mtu akikuuliza hiyo utaweza kumjibu? Na nyinyi mnaonaje?

**Audience:** Hiyo ni sawa, tunakubaliana.

**Com. Salome Muigai:** Tuangalie sura ya tisa, mfumo wa mahakama na sheria sehemu ya kwanza mfumo wa mahakama. Inazungumzia juu ya uwezo wa mahakama, msongwe wa mahakama, msongwe ni nini? Mnatafsiri kwani mimi ni mwalimu mzuri na tena ingali ninawakubalisha kuangalia kitabu, ukienda kusomeshwa na Mwalimu Beatrice hautakubalishwa kuona kitabu. What is msofara wa mahakama in Engilish? Hireachy yaani mahamama itatitiwa kwa ofisi, inazungumzia pia uhuru wa mahakama na tumeweka Supreme Court ama koti ya juu, hii ni pendekezo lenye haliko kwenye Katiba yetu leo, ni pendekezo mpya kuwa tuwe na koti ya juu, Supreme court. Kazi yake itakuwa nini ndio wenye itakuwa na mwisho wa rufani, it is the end na pia itafanya kazi la kikatiba ndio ukiwa na shauri ama na swali juu ya Katiba utaleta moja kwa moja kwa Supreme Court. Halafu kuna koti zingine kuna koti ya mahakama ya juu, kuna koti ya rufani, kuna koti zingine za Magistrate na pia tuna koti ya Kadhi. Nimeshaeleza kwa nini tuna koti za Kadhi, si hivyo wakati nilieleza habari ya dini.

Sehemu ya pili ni mfumo wa sheria. Pia wananchi wengi wajua kutenganisha ofisi ya mkuu wa sheria ama mwanasheria mkuu, tunamuita Attorney General, mwanasheria mkuu kwani tumeelezwa kuwa kuita mtu mkuu wa sheria ni kuonekana yeye ni kuu kuliko sheria, kwa hivyo hakuna mkuu wa sheria lakini kuna mwanasheria mkuu. (murmur). Kiswahili tumeletewa na wasomi hiki. Sasa tumetenganisha ofisi ya mwanasheria mkuu ambaye kazi yake kubwa ni ya nini, ni kushauri serikali kisheria na tumetenganisha ofisi hiyo na mkurugenzi wa mashtaka ya uma, public prosecutor. Kwani wakati mwingine hizo ofisi mbili unaleta utatanishi, wewe unataka kuishtaki serikali na kumbe mshauri mkuu wa serikali ndio mshauri mkuu. Sasa pamekuwa na conflict of interest. Sasa tumezifanya kuwa ofisi mbili yenye zitakuwa tofauti. Pia tuna wakili wa uma, wakili wa uma anaitwa nini kwa Kiingereza?

**Audience:** Public Defender.

**Com. Salome Muigai:** Publi Defender, mwenye atakulinda wewe mwananchi wa kawaida ukisikia umshtakiwa kwa njia isiyo ya kweli ama umetatizika kisheria kwa njia moja ama nyingine, tumeweka hiyo ofisi. Ni kama ofisi ya Ombudsman. Ni ya kulinda nani, wananchi na wananchi ni nani. Sema ni ya kunilinda mimi kwani ikiwa ofisi ni ya kulinda wananchi ije nitawacha ibomolewe juu ya wananchi lakini ikiwa hiyo ofisi ni ya kulinda mimi ije kubomolewa nitafanya nini, nitailinda. Kwa hivyo tuanze kuwekea mkazo kuwa hii mambo ni yangu na yako hawa wananchi sijuhi ni akina nani yenye kila mara tunasema ni ya wananchi. Mwananchi ni nani, ni mimi na wewe. Nimesema habari ya clemency of clemence of national mercy, uwezo wa kuhurumia hiyo unaweza pia kusoma.

Sehemu ya tatu ni juu ya taluma ya sheria na hiyo ndio mwisho wa sura ya?

**Audience:** Ya tisa.

**Com. Salome Muigai:** Ya tisa, naona hamlali na pia njaa haijawaumiza too much.

Sura ya kumi ni upunguzaji na uzambazaji wa madaraka yaani devolution. Wakati huu watu walituambia hiyo serikali ya Nairobi iko mbali sana na sisi, nikienda kutafuta title deed wakati mwingine nahitaji kuuza kipande cha hiyo shamba ndio nipata nauli ya kuenda wapi? Nairobi. Tunataka serikali yenye iko karibu na sisi. Sasa tumepeana mapendekezo ya kuwa na serikali iliyokaribu na watu hii serikali itaanzia kwenye kijiji. Kijiji kitakuwa na serikali yake halafu itaendelea katika kata, location itakuwa na serikali yake yenye itachaguliwa na watu. Halafu itaenda wapi? Wilaya. Serikali ile muhimu itakuwa ya wilaya. Kwa sababu gani? Kwa sababu kila wilaya na matako yako ni tofauti na wilaya nyingine. Kwa mfano serikali kama ikiwekwa hapa Uashin Ngishu jambo ile la muhimu kuliko yote itakuwa ni nini?

**Audience:** Ukulima.

**Com. Salome Muigai:** Ukulima, ukiweka serikali Garisa unafikiri ukulima itakuwa ndio matako yao pia ya kwanza? La. Ukiweka serikali Kajiado jambo lao la muhimu itakuwa ufugaji na pia hata tukienda zaidi ya hapo, tukisema serikali iko wilaya ya Uasin Gishu ukulima itakuwa ni la muhimu lakini itakuwa ukulima wa nini?

**Audience:** Wa ngano na mahindi.

**Com. Salome Muigai:** Wa ngano na mahindi lakini unafikiri tukienda Trans Nzoia itakuwa ukulima wa nini yenye tutapata huko?

**Audience:** Wa mahindi.

**Com. Salome Muigai:** Wa mahindi. Sasa unaona hata kwenye ukulima watu watakuwa na tofauti. Pengine tukienda Kiambu ukulima utakuwa wa nini, wa kahawa na majani. Unaona. Tukienda Kericho itakuwa ya nini, ya majani na ng'ombe ndio tunasema ile serikali ya chini na ya kutekeleza ile mahitaji ya wananchi itakuwa kwenye wilaya ndio ihudumie wilaya na mambo yake ya kipekee.

Halafu mkoa itakuwa na serikali sio kubwa kama ya wilaya kwani serikali ya mkoa itakuwa kazi yake ni coordination. Ku-coordinate ni kufanya nini? Kushirikisha. Kama watu wa Uasin Gishu wana ngano, wana mahindi hawana kitu cha kufanya nayo na watu wa kutoka Kajiado ambao pia ni wafugaji nao hawana mahindi serikali ya mkoa itatatufa soko kutoka wilaya ya Uasin Gishu kupeleka wapi, Kajiado nao watu wa wilaya wa Uasin Gishu kwani ngombe zao ni za nini, si ni za maziwa? Wataletewa nyama kutoka wapi? Kajiado. Kwa hivyo kazi ya mkoa itakuwa kazi ya coordination. Halafu national, kitaifa itakuwa ya kuangalia mambo fulani. Kwa mfano mambo ya usalama wa nchi lazima ifanywe kwa pamoja, si hivyo? Kwa hivyo itafanya hivyo. Mambo ya ushirikishi kati ya taifa letu na mataifa mengine itakuwa kwa pamoja na mambo mengine kama hayo, kwa hivyo tutakuwa na serikali katika kila kiwango yeye kutetea matakwa tofauti na hiyo ina sura nzima kuhusu devolution. Tafadhali msome kwa dhati ukajue pahali uko na vile unaendelea kufaidika.

Sura ya kumi na moja inaangalia habari ya ardhi na mali, mifumo ya sera za ardhi, umiliki wa ardh, uwandikishaji wa ardhi, awamu za ardhi, ulinzi wa mali katika ardhi na katika ardhi na kuanzisha Tume ya kifaifa ya ardhi. Jambo moja ningetaka kusema ni kuwa kila pahali tulienda wananchi wanashida kubwa kubwa juu ya nini? Ya ardhi. Tumeona sisi kama Tume hata tukikaa miaka miwili hatutaweza kusuruisha hayo mambo yote. Vile tumefanya ni kuwa tumeweka Tume ya kikatiba yenye imewekwa kwa Katiba. Yaani hii Tume haitakuwa ikilia afterwords, it should be kila pahali, yenye tulienda kama Tume tuliambiwa lazima tukuwe na land katika Katiba, lazima iwe entrenched. Kwa hivyo hii Tume ya ardhi tunaifanya entrenchment from the word go, it is the Constitution ndio iwe na mamlaka ya kuchunguza shida zilizoko na wananchi juu ya ardhi na mashamba lakini pia hii ndio tumesema juu ya ardhi yenye nimesoma kwenye hii Katiba. Ya kwanza tulisema kuwa ardhi ni mali ya Wakenya, sio mali ya serikali. The land does not belong to the government it belongs to the people of Kenya. Kwa hivyo kutakuwa na mashamba ya binafsi, kutakuwa na mashamba ya jamii na kutakuwa na mashamba ya uma na kutakuwa na masharti tofauti kuhusu hii mashamba. Tumesema pia Katiba hii italinda ardhi ya kila mtu so long as, unafikiria italindwa ikiwa imefanya nini? Iwe ilipatikana kwa njia ya halali. Soma hicho kiwango cha ardhi kina mambo muhimu ya itaji kujulikana.

Pia tumesema habari ya mazingira, tumesema Katiba hii yetu ni yetu na nani?

**Audience:** Na vizazi vijavyo.

**Com. Salome Muigai:** Na vizazi vijavyo. Sasa hizi vizazi vitakaa wapi? Lazima hivi vizazi vitakaa Kenya na lazima tuhifadhi

Kenya ndio hivi vizazi viikute. Si hivyo? Kwa hivyo Tume imeweka utaratibu wa ulinzi wa mazingira na tumeweka pia Tume ya taifa yenye itafanya nini, kusimamia mazingira na iwe Tume ya kikatiba already entrenched watu wasiwe wana….wawili au watatu ndio tulinde mazingira yetu. Tumezungumzia pia habari ya utekelezaji wa haki za mazingira na sheria za nini? Za mazingira.

Sura ya kumi na tatu inazungumzia juu ya fedha za uma na usimamizi wa ma-councils. Hii ni hali ya vile pesa za uma zinavyookotwa, ni habari ya kodi, ni nani atakayesimamia hayo mambo yote na utaratibu gani utafuatwa kutumia pesa za uma. Jambo moja geni ni lipi. Lunasema utoshaji wa ushuru lazima uambatane na huduma. Wananchi wakiwa wanatosha ushuru lazima nao wapatiwe hudumu na moja ni kwamba kuwa hiyo balance ikiondoka itaifanikisha nin? Ile nyingine? Kwa hivyo hio pia tayari ni sura yenye ingetakiwa mtu asome kwa makini.

Sura ya kumi na nne ni uduma za uma. Inazungumzia sehemu ya kwanza usimamizi wa ume, tume ya huduma ya uma, public service, mamlaka na wajibu na kuanzisha afisi na uteuzi wa maafisa wa uma. Tumezungumzia sana kuhusu maafisa wa uma. Lakini pia tumeweka kwenye haki za mwananchi kuwa ana haki ya huduma? Si hivyo? Tumeeleza pia lazima kodi yake iambatane na nini? Na huduma. Na wafanyikazi wa serikali lazima pia wahudumie wananchi kwa njia ya haki. Na ukisoma hiyo taaluma utaona ama hiyo tarifa na ufafanizi zote utaona mambo gani tumesema juu ya public service. Tumeweka pia huduma ya polisi. Tulipata malalamishi nyingi ya kusema kuwa polisi wanapokuja kufanya recruitment, yaani kufanya nini?

**Speaker:** Kuajiri.

**Com. Salome Muigai:** Kuajiri watu. Tulipata kama ni wazee ndio walilalamika kuwa watoto wao wanakimbia, wanahema, wanafanywa nini lakini mwishowe hawaoni nini? Matokeo. Hawaoni watoto wao wakifanya nini? Wakiajiriwa. Sasa kuna taaluma ya kuajiri polisi wenye watatuambia polisi wametoa wapi, ni nani atayeajiriwa kuwa polisi, wilaya fulani imetoka watu ngapi. Kuna mtu mwenye tutaulizwa sasa hiyo Tume na pia Tume ya kuajiri wafanyikazi wa uma tutaitakia hivyo. Kwa hivyo hatustaki kusikia kuwa TSC tumeifanya entrenched kwenye Katiba ili ikuwe bado ina uhuru wa kuajiri na kuwatumikia waalimu nayo pia inaweza kuulizwa swali ikiwa kuna swali juu ya waalimu.

Pia sehemu ya tatu inaangalia habari ya huduma ya Kenya ya kurekebisha tabia, kanuni na malengo yake. Kuanzisha huduma za Kenya za kurekebisha tabia, uteuzi wa mkurugenzi wa huduma ya Kenya ya kurekebisha tabi, hayo yote na habari ya magereza. Magereza, remand homes na vitu kama hivyo na ukisoma utaona tumependekeza hii.

Sura ya kumi na tano ni kikosi cha ulinzi wa usalama wa taifa. Hiyo tumezungumzia itakuwa na nani. Tumesema kuwa itakuwa inasimamiwa, mwenyekiti wake atakuwa Rais na ukiangalia utaona nani huwa wenzake.

Sura ya kumi na sita inazungumzia juu ya uongozi wa uaminifu. Wananchi wengi walitueleza kuwa haitoshi kuwa mtu amesoma

walisema kwanza tunataka watawala wa Kenya wamesoma. Kwa hivyo tumesema mtu mwenye anataka kusimamia kiti cha Bunge lazima awe na kidato cha nne cha masomo lakini pia somo hiyo haitoshi tunataka pia kumjua yeye ana nidhamu vipi. Kwa hivyo tumeunda kikundi cha watu chenye kitaangalia habari ya uongozi wa uaminifu. Kwa hivyo kama wewe unataka kuwa kiongozi itakubidi kuchunguzwa habari ya mienendo na maadiri yako ndio ukubalike kuwa kiongozi.

Sura ya kumi na saba ni Tume za Kikatiba, tumezungumzia Tume fulani. Nitazungumzia kwa kifupi zenye sijazungumzia, moja ni kanuni za kuunda Tume, malengo na uhuru wa Tume lenye zitakapoundwa Kikatiba, vipi vitashirikishwa na waliomo kwenye Tume watakuwa nani. What do you need to qualify as a Commissioner in different commissions. Pia itakubidi kuwa na utaalam na pia nidhamu ya kukubalika na watu. Tumezungumzia Tume kadha wa kadha, tumesema hizi Tume zote lazima zipatiwa pesa zao kando ndio waweze kufanya wajibu wao na tumesema kuwa kila mwaka, kila Tume itakuwa inajulika kila mwaka kutoa repoti yao kwa wananchi kupitia Bunge ndio tujue ilikuwa inafanya kazi gani, imefikisha wapi, inashida zipi, kwa nini haijamaliza kazi yenye tuliituma kufanya.

Tutakuwa na Tume moja ya Kikatiba itakaa kwa miaka tano peke yake. Kazi yake ni kuakikisha haki baada ya miaka tano kila sheria yenye iko Kenya imeambatana na Katiba yetu. Ikishamaliza kazi yake baada ya miaka tano imemaliza kazi yake mwisho. Tutakuwa pia na Tume ya haki za binadamu na haki za kitawala hiyo pia ni ya kuchunguza, kuhakikisha kuwa masilahi ya kila mtu na haki zake hazigeukwi na mtu binafsi wala na shirika lolote na uisi kuwa haki zako zimegeukwa una haki ya kuenda kwenye Tume. Moja ya kazi ya hii Tume pia itakuwa kuangalia usawa wa kijinsia kuhakikisha kuwa wanawake watashirikishwa kwenye utawala katika sehemu zote na viwango vyote vya utawala. Pia kutakuwa na Tume moja kazi yake itakuwa kuangalia haki za watoto, watoto wetu wanashirikiwa vipi. Itakuwa kazi yake pia ni kuangalia haki za walemavu zinatiliwa maanani kivipi. Kwa hivyo tukisema lazima kila kikao, tumesema kwenye haki za walemavu kwa mfano, kuwa wanahaki ya kuwakilishwa katika sehemu zote za uongozi. Ikiwa kijiji chako kimeweka baraza lao inalinda mlemavu yoyote basi pahali ya kuenda ni kwenye hii Tume na huyu mwenye hii Tume ana haki ya kusema hilo baraza halijaundwa kihalali kwamba hakifuatana na Katiba na kitu chochote chenye hakifuatani na Katiba kiko out, ndio wanatoka wakasema kiko nini? Kwenye kandanda tunasema kiko ni nini, off side.

Pia tutakuwa na Tume hii ya uadilifu na uaminifu yenye itachunguza taabia za wale wenye kutaka uongozi. Pia kila mmoja aneyetaka kuongoza lazima a-declare their wealth. Utuambie wewe una gari ngapi, una ng'ombe ngapi, una nini na nini na nini. Mwishoni baada ya kumaliza kututumikia tutafanya audit tena tutasema sisi tulikuwa tunakupata shilingi elfu mbili, tunaona una gari sita na kila moja ni ya milioni mbili na kadhalika, utueleze.

Kutakuwa na Tume ya mishahara na malipo, hii Tume kazi yake ni kuangalia mishahara ili mtu mmoja asipate milioni nne na mwingine apate mia nne kwa mwezi na wakienda Uchumi wananunua unga bei…

**Audience:** Moja.

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo itaangalia mishahara ya kila mtu ili kuweza kuangalia kuwa sio kusawawisha lakini kuhakikisha kila mtu anapata mshahara yenye kumpa yeye maisha ya kibinadamu yenye heshima za kibinadamu. Kutakuwa pia na Tume ya huduma ya waalimu, kama vile nilivyosema na tutakuwa na Tume ya Kikatiba yenye tumeshazungumzia na tutakuwa na kikundi ya Kikatiba yenye kupokea malalamishi juu ya Katiba. Kwa hivyo pahali pa kulalamika ni pahali pengi na hazijakaa tu Nairobi, tumefanya devolution, tumefanya decentralization kwa hivyo zitapatikana pahali karibu na mahali mwananchi anapokaa.

Sura ya kumi na nane ni kubadilisha Katiba, tumesema kuwa mabadiliko ya Katiba ni kwa utaratibu na kwa hivyo tumeifanyia mipango kabambe kwenye hii sura ili kubadilisha Katiba kusiwe na pengo. Hatutaki kusema kutoka leo kitu fulani haifanyiki ama ofisi fulani aiko na kumbe hatujaweka ofisi nyingine tayari kuwapatia wananchi huduma. Kwa hivyo ukisoma hiyo sura utapata tunataka mabadilisho gani ya Kikatiba, mabadilisho ya Bunge na haki ya utiifu pia tumeleta kwenye hiyo sura.

Sura ya kumi na tisa ni ufafanuzi, nilisema kila jambo yenye unaweka kwa sheria ni lazima ufanye nini? Ufafanue kwa hivyo hapo kuna ufafanuzi katika sura ya kumi na tisa.

Na sura ya ishirini ni kanuni za mifito na matokeo, sorry hiyo ndio pahali tumeweka utaratibu wa kubadilisha. Hii ya kwanza ni haki ya kubadilisha kwa Katiba lakini hii ni nyingine ni utaratibu tutakaofuata ili kubadilisha. Smoothly, harmonious transition. These are the provisions for the transition kutoka kwa Katiba iliyoko sasa mpaka kwa Katiba mpya na kwa hayo mengi wakazi wa kikao cha Bunge cha Eldoret ya Mashariki hiyo ndio Katiba yenye tunawapendekezea. Asante sana.

Na sasa tutaenda kwenye taratibu nyingine na hiyo itakuwa wakati wa kuuliza maswali. Ningetaka kusema mambo mawili kama hamjaniuliza maswali, kuna swali nitalijibu kabla sijaulizwa. Je, jambo la pili kutokea hapa ni nini? Jambo la pili kutokea hapa ni Kikao cha Kitaifa cha Kuzungumzia haya maswala yaani tukubaliane, tunajaribu kubaliana kitaifa. Kwa hivyo kila wilaya itasimamiwa ama itawakilishwa na watu watatu. Moja lazima awe mwanamke, ile uchaguzi yenye tulizungumzia leo tuna bahati ya kuwa na mmoja wa mwakilishaji wetu, Mwalimu simama tena wakuone wengine walikuja kama umeshazungumza.

**Speaker:** …(Inaudible)

**Com. Salome Muigai:** Aaah, okay can I have the district delegates wenye wako, kwa hivyo leo tuna delegates wawili. Delagate mmoja mama na delegate mmoja baba na tuna mwingine mwenye halipo hajuko hapa. Zaidi ya hawa wawili pia, NGO Council itapatia Uasin Gishu wakilishi wawili, mmoja ni rafiki yangu sana anaitwa Samuel Tororei kwa hivyo anajua ana constituency yake hapa katika watu wenye ulemavu na pia atakuwa mwakilishi wa Wilaya ya Uasin Gishu na wapili alikuwa mama mwenye amechaguliwa sijuhi kama ingali anakuja, alikuwa na jambo moja ama mawili yenye alikuwa anaangalia. Sasa kwa hivyo Uasin Gishu wanakuwa na watu wangapi? Watano katika hii delegation. Kazi yao ni nini? Kazi yao ni kuwa

mkishawajua, mkishasoma hii Katiba mkubaliane nao pengine hata tumekubaliana hapa kuwa utaleta maoni yako ya ziada, ukiona kuna jambo lenye kabisa hukubaliani nalo ama kuna jambo la ziada ungetaka kuongeza. Uandike maoni yako ulete kwenye ofisi ya Coordinator yenye iko katika Library, mnaijua? Halafu hao wakilishi wenu watayasoma hayo matakwa yenu ndio wenye watakuja kuwakilisha. Yaani ukija kuwakilisha, huji kuwakilisha maoni yako wewe mwenyewe, unakuja kuwakilisha maoni ya wilaya yako. Kila mama mna mama mwenzenu, hebu simama tena mama na utueleze jina lako ulikuwa hauko.

**Emmy Kiprop:** Kwa majina naitwa Emmy Kiprop niko katika ofisi ya Katiba yenye iko kwa Library ukipata repoti yoyote utaileta kwenye . ….(Inaudible)

**Com. Salome Muigai:** Hiyo ni vizuri, kwa hivyo hao ndio wawakilishi wetu na kazi yao ni ya kuwakilisha nyinyi. Kukiwa na mambo fulani fulani utawaeleza wao, kwa hivyo leo ningetaka tu ufikirie habari ya kuelewa hii Katiba mniulize maswali yenye inahusiana na uelewe, so that you understand. Lakini kama kuna kitu yenye mngetaka kubadilisha muwaone nani, muwaone delegates wenu.

Jambo la pili ningetaka kujibu kabla sijaulizwa ni kuwa je, kikao hiki cha kitaifa kitakuwa na akina nani? Zaidi ya hawa delegates watatu kutoka kwa kila wilaya kutakuwa na Wanabunge na wanabunge ni wangapi? Mia mbili na?

**Audience:** Mia mbili.

**Com. Salome Muigai:** Mia mbili na kumi na ishirini na mbili, wote watakuwa huko. Zaidi ya hayo tutakuwa pia na watu wenye kuwakilisha ….tafadhali tusitoe vitabu vyote kuna watu wengine tunapelekea.

**Audience:** …(Inaudible)

**Com. Salome Muigai:** Ndio lakini na bado sijawapatia watu wa Eldoret North na sitaki kumalizia kila mtu na ndio ningesema kama Mr. Bor angepeana yeye mwenye ama Mr. Mitei ndio wenyewe wajue pia watagawanya, sisi wenyewe tukijichukulia huenda tukamalizia wengine. So tutakuwa na wahusika kutoka kwa NGO, civil society ndio walichagua Tororei na huyo mama mwingine. Wewe ulichaguliwa na…

**Emmy Kiprop:** District.

**Com. Salome Muigai:** District, okay mama yule mwingine ndio wa NGO Council. Basi nawaambia watakuwa na watu wao na pia hata akina mama hawakupata nafasi kupea wakina mama wengine kwa njia huo. N.G.O. Council imetupatia watu watatu wenye ulemavu na hawa wote ni akina mama kwa hivyo huenda tukapata hiyo tukasema pia akina mama wanaulemavu

na wanashida zao za kipekee zenye akina baba wenye ulemavu hawaelewi hata kidogo. Siku moja umebaba mtoto kwa tumbo na bado uko kwa hicho kitu cha …ama kwa classroom. Pia tunapata shida zingine za pekee zenye mama mwingine tu ndio anaweza kuelewa, kwa hivyo wamama wenye ulemavu pia kuhusishwa. Basi hawa watu wote watapigana watakuwa wako…..(Inaudible) nafikiri hii ndio meeting itakuwa kubwa Kenya imetiwa kisiasa, watakuwa wakilishi zaidi ya 600. Tumewapa nafasi wa kuzungumza kwa muda kama mwezi moja hivi ndio wakubaliane, wakikubaliana kwenye hii Katiba basi itaenda Bunge na kazi ya Bunge itakuwa kufanya nini, kuisilisha tu. Bunge lazima waikubali kwa jumla ama waikatae kwa jumla hawakubalishwi kutoa sehemu yoyote.

Swali gani lengine nimeulizwa kila pahali yenye nimeenda? Je, Bunge ikivunjwa kabla ya hiyo mikutano itafanyikaje, your guess is as good as mine. Hilo ni jambo lenye ninajua mtu anaweza kutapata ni makosa kufanyika na huenda tukakosa kuwa na Katiba mpya kwa hivyo tutaenda kwa Wabunge wetu tumwambie wajaribu kutovunja Bunge mpaka tukuwe na Katiba mpya. Sasa ninachukua maswali na nitamwacha Bwana Juma ashikilie ushukani kwa muda muinue mkono mwenye ana swali na mimi nitaandika maswali ya watu kama kumi hivi ndio nipate nafasi ya kupumzisha sauti yangu mtakaponiuliza maswali. Bwana Juma.

**Dan Juma:** Thank you very much Commissioner, the first ten questions.

**Com. Salome Muigai:** Juma hana sauti yenye….(Inaudible) Juma ni wakili sio mwalimu kama mimi.

**Dan Juma:** Okay, alivyosema mtauliza maswali ili mjue more about what she told us. So you are going to be as brief as possible. So we are going to take the first ten questions. One of the members of the committee should come and make sure they put their names in that register. Inua mkono kama unataka kuongea, hawa ni watatu, wa nne, tano.

**Com. Salome Muigai:** ..(Inaudible)

**Dan Juma:** Yes, na ukipata kama swali lako limeulizwa usirudie, kwa hivyo nenda pale na ujiandikishe hapo.

**Com. Salome Muigai:** Mmoja wa committee mngekuja kusaidia mmoja wa kuandikisha watu.

**Dan Juma:** Wenye wamechaguliwa wakuje na wapange laini hapo.

**Com. Salome Muigai:** Chukua kitabu chenye kiko pale, uliza swali lako kwanza kabla ya kujiandikisha.

**Dan Juma:** Tutapewa majina kama vile ….(Inaudible)

**Com. Salome Muigai:** Wale watu sita wenye waliitwa wakuja hapa mbele. Ulikuwa number one, simama pale, kwa hivyo

uliza swali lako na unasema jina lako.

**John Kariega:** Madam Commissioner na wale wanashirikiana naye, kwa majina yangu ni John Kariega na ninahusika upande wa CKPC katika Kanisa Katholiki, katika jimbo hili na ninatoka upande wa Kapsoya. Maswali yangu ni machache tu Madam Commissioner na ya kwanza iko katika kipengele cha mia moja na sita ambao ni kuhusu members of the National Council. Ninautatanishi kidogo kulingana na hawa watu vile watakavyochaguliwa na wakati ulikuwa ukiendelea ulisema thelathini watakuwa akina mama na wengine hawa sabini nikakosa kuelewa hawa watakuwa ndio wazee au pia watachanganyikana pale na pia watachaguliwa kivipi.

Swali langu la pili pia ni katika kipengele 107, mia moja na saba juu ya National Assembly. Hiyo ya National Council nilikosa pia kuelewa wanasemaje kuhusu single members katika constituency.

**Com. Salome Muigai:** Single…

**John Kariega:** Single members.

**Com. Salome Muigai:** What do you mean by that?

**John Kariega:** 106 (a) of 70 members on the basisi of single member constituency. Sikuelewa mahala pale halafu ndio sasa naingia hiyo ingine ya National Assembly, Nilikuwa nikiuliza swali nikijibu kidogo pale wakati ulikuwa ukiongea kuhusu sehemu ambazo zina wakilishi Bungeni wengi na sehemu zingine zina wakilishi wachache na kwa sababu Katiba hii inasema ya kwamba constituencies zenye ziko ndizo bado zitakua recognized na hii Katiba. Je, swali langu liko kwamba ni muda gani itachukuliwa ili kuweza kusawasisha kwa sababu sehemu zingine zilichaguliwa kisiasa.

Halafu swali lingine iko katika sehemu ya 233, ni katika chapter 11, hali ya mashamba. Naye katika sehemu hii ni kuhusu wale wanaosemekana ndio wenye ardhi naye swali langu lilikuwa nilitaka kujua je katika wale wako na mashamba kwa wakati huu na hao wamemiliki ardhi kwa wakati huu na pengine ilikuwa imechukuliwa kisiasa. Je ni kwa sababu Katiba hii inasema ya kwamba ardhi ile wakati Katiba hii itakuwa ikitumika ardhi yoyote ambayo ilikuwa ya mwenyewe itabaki kuwa hivyo hivyo, je pale katika mashamba ya uma itakuwaje?

Naye kifungu kingine nilikuwa na tashwishi nayo ni 234, nayo nilikuwa na swali kuhusu, kukiwa kuna mgeni ambaye ako na kipande cha shamba cha uma ambaye anakifanyisha kazi , atakuwa akikilipia na kama ni kulipia pesa zile zitakuwa zikienda mifuko gani na zitakuwa zikitumika katika kazi gani. Nafikiri ni hayo tu Madam Commissioner. Asante.

**Chrispinus Munako:** Hamjambo Commissioner. Nilikuwa nauliza…

**Com. Salome Muigai:** Jina.

**Chrispinus Munako:** Kwa jina naitwa Chrispinus Munako.

**Com. Salome Muigai:** Endelea.

**Chrispinus Munako:** Nilikuwa nauliza kama waziri atafutwa kazi itakuwa sasa anarudi kuwa Mbunge ama watabadilishana Mbunge awe waziri na waziri awe Mbunge. Halafu nilikuwa nauliza kama rangi ya national flag Wazungu wameweza kujumuishwa kwa hiyo white colour na wale walipigania uhuru hawaja jumuishwa. Kwa mfano wanajumuhishwa na rangi gani katika hiyo national flag? Ni hayo tu.

**Com. Salome Muigai:** Asante, kama umemaliza tafadhali patia mwenzako. Basi tuende kwa haraka ili kila mtu apate nafasi.

**Wilfred Gethusi:** Mimi swali langu ni juu ya percentage ambayo imepewa kwa wanawake kwa wakilishi.

**Com. Salome Muigai:** Utuambie jina lako tafadhali.

**Wilfred Gethesi:** Jina langu naitwa Wilfred Gethusi.

**Com. Salome Muigai:** Gethusi, haya endelea.

**Wilfred Gethusi:** Sasa hii percentage ambayo imepeanwa kwa wanawake tunaambiwa kwamba wamepewa a third na isipotosha sasa hivyo viti vingine vitaenda wapi?

**Com. Salome Muigai:** Katika nini?

**Wilfred Gethusi:** Ikiwa wanawake hawata patikana wenye wanafurahia kujiingiza kwenye hiyo halafu wasitoshe nambari ambayo wamepewa hivyo vitu vingine vikibaki vitaenda wapi? (***Laughter)***

**Isaack Kotut:** Basi kwa majina naitwa Isaack Kotut na ningependa niulize swali kuhusu representation na decision making na walemavu.

**Com. Salome Muigai:** Jina lako?

**Isaack Kotut:** Nimesema Isaack Kotut. Ya kwanza ni kwamba katika Parliament yetu, mambo ya wanawake ya kwamba wamepewa one third lakini hukusema walemavu watapewa kiasi gani na vijana hio ni sehemu mbili ambayo mlipounda Katiba mlisahau.

Basi ya pili tunasema ya kwamba hii devolution of power from the village na kuendelea wale ambao watachaguliwa kutoka villege, district mpaka provincial watakuwa wakipata mishahara? Tena ningependa kushukuru wakilishi wetu wa district ya kwamba wako pamoja na sisi na wanasikia yale ambayo tunasema na tunauliza maswali ili waweze kuenda kuchangia huko na ningependa kusema tu yale ambayo yanatoka kwa NGO, ya kwamba kama mtu si active hajaanza kwa mashinani mbona anachaguliwa aende national conference na hakuhusika kwa constituencies kusikia maoni ya watu walikuwa wanasema nini na nini lakini amechaguliwa aende national conference, atapata wapi maneno? Asante.

**Daniel Kimutai:** Naitwa Danie Kimutai Rambae natoka Kapsoya, niko na maswali mawili, ya kwanza ni kutoka chapter 20 (iv) majorly it concerns marriage. Ukisoma…

**Com. Salome Muigai:** Tupe jina lako tena.

**Danie Kimutai:** Jina ni Daniel Kimutai Rambae. Swali langu linahusu marriage, ukisoma chapter 20 (i) inasema tu kuhusu watu wenye wamekuwa married then chapter 38 (iv) inaongea kuhusu parties to a marriage na Constitution haituambii marriage ni kati ya nani na nani imewacha tu hivyo. Now I am foreseeing a situation where two men can try to marry, yes because that is how it is here. So I would have suggested that may be an interpretation should be put after that chapter to interprete that marriage is between so and so.

My second question would have come from this, there was an article on the election of the President. Now I don't see how this will work, I can only see that there will be a lot of work especially….(Inaudible) in that the President is going to be elected between five Presidents at the same time the Prime Ministers is also going to the elected by the same … At the same time immediately after election ni kama he is not supposed to be a member of a political party. So my suggestion would have been, why don't we only elect the Prime Minister tuachane na Rais and then parliamentarians wakutane in Parliament and to come to a consensus, let them elect the person to be the President rather than the President going through a lot of exercises here and there.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana. Yaani sitaki kukukatisha lakini hii si wakati wa kutoa maoni, maoni unatolea delegate wako, mimi unaniuliza maswali ya ufafanuzi ile huelewi.

**Daniel Kimutai:** Okay, …..(Inaudible). Thank you.

**Abdul Tuwen:** Basi hamjambo?

**Audience:** Hatujambo.

**Abdul Tuwen:** Mimi ni Abdul Tuwen kutoka Eldoret. Nataka kuguzia swali kuhusu watoto. Nimeona kuwa watoto wanataka ulinzi kwa hii Katiba lakini haikufafanuliwa vizuri kuhusiana na watoto wenye wamezaliwa nje ya ndoa. Imeandikwa kwa ukweli kuwa lazima watunzwe, mtu anaoa bibi mmoja halafu nje nje amezaa watoto wengi who will be responsible for taken care of those children. Nimesikia ni lazima watoto walindwe, hapo ndio ningetaka mfanye marekebisho kidogo.

Swali la pili.

**Com. Salome Muigai:** Hilo ni swali ama ni maoni?

**Abdul Tuwen:** Ni kama ni swali.

**Com. Salome Muigai:** Endelea tu.

**Abdul Tuwen:** Swali la pili ni kuhusu devoulved government kuhusiana na mkulima. Inaweza kuwa wananchi watashindwa kuchagua viongozi wenye maoni kuhusiana na hali katika eneo letu, sasa ninaona ingefaa hii federal government isianzishwe mahali penye inausiana na ….(Inaudible). Kwa vile juzi tulitoa maoni kuhusiana na hali hii na nimeona imewekwa chini katika devolved government. Ni hayo tu. Asanteni.

**William Oleseur:** Madam Commissioner, swali langu.

**Com. Salome Muigai:** Jina lako kwanza.

**William Olesur:** Jina langu ni William Oleseur. Swali langu linahusiana na persons with disabilities kifungu cha thelathini na tisa (ii) D, access to public places katika kitabu hiki. Ningetaka vile kifungu imeandikwa hapo public places lakini ukiangalia pahali kama hall hii ama …(Inaudible). Hapa imewekwa katika Katiba lakini tutafanya namna gani ili kurekebisha pahali kama hapo kwa sababu hii building ilikuwa imejengwa bila kufikiria juu ya wenzetu wasiojiweza. Na wenzetu watakuwa wanaingia hapa lakini haijajengwa kulingana na…(Inaudible).

Kwa (h), disability materials kama wheelchairs, fimbo ya vipovu hazipatikani hapa katika Eldoret na itakuwa ngumu na gharama nyingi kununua. Kwa hivyo ningetaka vitu kama hivyo viwe decentralized na kuwekwa mahali kama ….na kama inawezekana iwe ikiwa imported isiwe na tax, iwe tax free.

**Com. Salome Muigai:** Unaniuliza maswali ama unanipa maoni ama ni hayo mawili? Lazima ufuate Tororei umpe maoni na mimi uniulize maswali ya ufafanuzi.

**William Oleseur:** Asante sana nimeelewa nitampatia Tororei hayo maswali. Vile tulikuwa tunaongea juu ya yale ambaye tulikuwa tumeandika …..(Inaudible).

**Com. Salome Muigai:** Nitajibu hayo maswali yenye mmeshauliza halafu ndio nitapatiana nafasi tena watu wengine sita ama zaidi kuuliza maswali. Nitaanzia na swali la habari ya ministers, je minister akitolewa kwa kazi atarudi kuwa MP. Ministers, tutakuwa na u-minister mara mbili, mmoja atakuwa ameajiriwa moja kwa moja kwa Bunge Amerika ndio lina swala kama hilo hawachagui waziri kutoka kwa Wabunge na akifutwa basi amefutwa. Je, jaji mwenye alikuwa magistrate akipelekwa kuwa Judge, akiandikwa kama Judge anarudi kuwa magistrate? La. Kwa hivyo hilo njia ….lenye mtu amefanywa kuwa minister ama hiyo ni kazi yake ya uwaziri na hakuna hali ya kuingia tu kuwa mtu yeyote mwingine hata akiwa alitoka Bunge, akijiuzulu kuwa Mbunge tunaenda kwa elections. Kunachaguliwa Mbunge mwingine ili aakilishe watu wa kikao hicho. Si hivyo? Sasa akitolewa kuwa Waziri atarudi Bunge akitaka nini na tayari ameshachukuliwa. Kwa hivyo ni chagua la watu tunafanya Wakenya waanze kuchagua kazi moja na uweke maanani hiyo kazi moja.

Alisema bendera haina ….ati ile rangi nyeupe ni ya nani, ni ya Wazungu. Eeh, ni kwamba si rangi nyeupe ilikuwa ya umoja wetu, kulikuwa na peace. Ilikuwa ni ya amani sasa umeweka ni ya Wazungu?

**Chrispinus Munako:** Ziko mbili moja ni ….

**Com. Salome Muigai:** Hakuna pahali yenye tulisikia hiyo, wakati tulipata uhuru wale wenye tulikuwa pale shuleni na mimi nilikuwa nasoma Township, tulikuwa tunaimba wimbo wa kuonyeshana maana ya hizo rangi lakini ilikuwa hakuna ya Mzungu kwa hivyo ni amani yetu na umoja wetu. Lakini ukiwa na maoni ya ziadi basi mpe jirani yako pale anaenda kwenye kikao cha taifa.

Wilfred anauliza juu ya hii percentage ya wanawake, wanawake wakiwa na 30% kwa Bunge, hii Bunge itakuwa na watu chini ya mia tatu kwa hivyo ikiwa wanawake ni theluthi watakuwa wangapi?

**Audience:** Mia moja.

**Com. Salome Muigai:** Mia moja na wanawake kwa Kenya ni wangapi?

**Audience:** 51%.

**Com. Salome Muigai:** 51% percent ya milioni ngapi.

**Audience:** Thelathini.

**Com. Salome Muigai:** Thelathini, kwa hivyo ni milioni ngapi wanawake?

**Speaker:** …(Inaudible)

**Com. Salome Muigai:** At least milioni kumi na tisa sasa kwa nini wanaume ndio tunapinga kuwa kutakana na milioni kumi na tisa tutakosa wanawake mia moja. ***(Laughter).*** Sifikirii kama hiyo ndio shida, shida itakuwa wanawake wakitaka vitu nusu kwa nusu ama wakitaka 51%. Democracy inasema uwakilishwe kulingana na nambari zako kwa hivyo akina mama sijuhi kama watakuwa ama akina mama pia tutakuwa na shida kupata wanawake mia moja kupeleka Bunge?

**Speaker:** La.

**Com. Salome Muigai:** Isaack anauliza juu ya viti vya watu waliona ulemavu na vijana kuwa hazijawekwa kulingana, umpatie Tororei hiyo homework. Asikuambie akirudi kutoka Nairobi bila …..(inaudible) hata ….ama akuja akiwa na percentage. Yaani wakati wa kutengeneza Katiba ni shida sana kukumbuka kila kitu na kutia ndani ndio sasa tunaleta watu wenye wa kutengeneza waje watueleze pahali gani kuna pengo na kitu gani tutaweka kwenye hilo pengo. Tungefikiria ati Katiba inatosha basi tungesema ipelekwe kwa Bunge moja kwa moja lakini nafikiri bado kuna nafasi ya watu wengine kuchangia zaidi na kuifanya nzuri zaidi.

Naulizwa juu ya devolution watu watalipwa, viongozi wetu tukiwachagua tutawalipa. Kwanza kuna shida ya wakuwalipa? Tusipotumia fedha zetu vibaya kwa kupatia watu hongo na kuiba na kufanya nini, wakichukua fedha zetu na watupatie huduma na katika huduma na walipwe mishahara na ndio unaona tumeweka Tume ya mishahara, kwa hivyo itaangalia mishahara gani itawezekana kwa uchumu huu ulioyoko kwa vitengo hivi mbali mbali. Wakati uchumu wetu utaenda juu hatutaki tuende chini zaidi, mnataka ya chini?

**Audience:** La.

**Com. Salome Muigai:** La. Kwa hivyo ikienda juu zaidi basi hii Tume pia itafikiria habari ya mishahara kuenda juu. Nimeulizwa kwa nini Mjumbe mwenye hajajishugulisha na mashinani amepelekwa kuenda kwenye taifa. Basi lazima uwaulize watu wa Uasin Gishu kwani tulileta hii hapa mjichagulie mwenyewe, ni mtu wa Council.

**Isaack Kotut:** We did not play any role walichagua hawa tu mama mmoja na wanaume wawili.

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo unafikiria NGO hawajuhi vile wanafanya?

**Isaack Kotut:** Yes. ***(Laughter)***

**Com. Salome Muigai:** Unajua ni vile sisi pia tumepatiwa nafasi ya kuwachagua viongozi, si hivyo? Tukiwachagua viongozi wasio wazuri hiyo jukumu ni ya nani? Ni yetu sisi tumepatiwa fursa. Yes, you have the privilege ya kuitumia na ukitumia vibaya na ukisikia tuna …..(Inaudible) inatosha miaka tano ya kutowakilishwa basi lahaula. Ama mnaonaje? Kwa hivyo ni sisi kila mtu kuanza kufikiria tuulize watu wa NGO hapa. Ukiniuliza mimi sitaweza kujibu hilo swali kwani sisi kama Wanatume hatukuchagua hawa waakilishi tumewapa nyinyi jukumu na fursa ya kuwachagua. Nyinyi ndio mtuelezeni mliwachaguaje?

Daniel Kimtai, marriage…..wapi Mjumbe wenu, mwambie ungetaka ufafanuzi zaidi juu ya hiyo. Kuchaguliwa kwa President una tashwishi nayo, fanya mapendekezo yako kwa Mjumbe wenu. Lakini kwani Rais kwanza ndio mwenye atakuwa mwenye kulinda Katiba na ndio mwenye atakuwa kazi yake kubwa ni ya kupatanisha Wakenya wa jamii mbali mbali ili tuwe pamoja. Kwa hivyo ninaona mimi ni lazima achaguliwe na sisi ndio asipotupatanisha tumuuliza kwani ulitupatia nini na tulikupa kazi ya kufanya nini, ya kutupatanisha. Akichaguliwa kwa Bunge peke yake itakuwa haitabidi kufikiria anatutumikia sisi moja kwa moja na Raisi ndio mwenye atatupatanisha na mataifa mengine ya kitaifa, pia atatusimamia na kuangalia misimamo wetu. Akiwa hatukumchagua sisi wenyewe basi tunaakilishwa na mtu mwenye hatukumchagua. Kwa hivyo sijuhi wengine wanaona nini, tumchague Rais ama tuache Rais achaguliwe na Bunge. Kwa sababu gani tunasema Prime Minister achaguliwe na Bunge, kwani ni mkubwa anasimamia serikali na serikali inaangaliwa na wananchi na wananchi wenye tumechagua ni nani, ni Wanabunge. Unaona huo husiano, hata jambo moja. Lingine lenye watu walisema hawataki Waziri watoke Bunge ilikuwa Bunge inatakiwa kuangalia serikali na kuikazia macho ione inafanya kazi gani. Kwa hivyo ikiwa Wabunge wengine ni wa serikali wananchi walikuwa na tatizo kuwa hawachungi serikali kwani hao wako katika serikali. Kwa hivyo sasa tuligawanya hayo mamlaka. Ijapokuwa kazi ya Bunge ni kuchunguza Waziri Mkuu na serikali yake vile inavyofanya na wanaweza kugiga kura ya kutokuwa na imani na huyo Waziri Mkuu waliyemchagua.

Abdul anataka kujua habari ya watoto wenye wamezaliwa nje ya ndoa. Tumesema kila mtoto ana haki ya kulindwa na kulindwa na kufanya nini? To be protected and provided for. Alindwe na afanyiwe nini?

**Audience:** Ahudumiwe.

**Com. Salome Muigai:** Ahudumiwe kwa hali na mali na mama yake na baba yake, wawe wameoana au hawajaona. Mtoto hana habari, mtoto akizaliwa ana habari kama nyinyi mmeona ama hamjaona, ana habari? La. Kwa hivyo yeye ana haki ya kulindwa na hawa wazazi wote, wawe wameoana ama hawajaoana. Hata wakiwa wameoana na waachane bado wana jukumu

ya kulea mtoto wao. Na hii mtu yeyote anaweza kuenda kotini kuwekwa maanani hilo ama mtoto mwenyewe. Mnajua according to the new children's Act mtoto anaweza kuenda kotini yeye mwenyewe moja kwa moja, akasema mama yake ama baba yake hajamtimizia matakwa yake na serikali itamsimamia. Tumeweka kwa Act na kuzungumzia kuwa, mtoto akiwa na kesi yoyote serikali itampatia wakili ili asimamiwe bila hata kuhitaji kulipa malipo yoyote. Hii Katiba mpya inasimamia mtoto vilivyo, ninaona akina baba tayari wameanza kuwa na shida. Huu ni wakati mpya, habari ya watoto serikali ama Katiba hii imeangalia kwa undani kabisa na siku hizi tuna DNA, kazi raisi tukienda pale Referal dakika mbili tukitoka huko tunakuambia wewe ndio baba ama wewe ndio mama. Pia wakati mwingine mama hawapata wajukuu wao kwa hivyo Katiba inawajulisha wazazi kulea watoto.

Alikuwa na shida sana kuwa pia katika serikali ya wilaya kutoa fedha ama sheria zinazofaa kilimo. Kama nyinyi mmechagua watu wa Uasin Gishu na ni wakaaji wa Uasin Gishu wakose kuwekea kilimo maanani wamewekea nini nyingine na hiyo ndio usalishaji wa mali katika eneo hii. Pia jambo moja lingine tulisema ni kuwa wananchi wanakazi ya kurudisha Mjumbe, kumrudisha kutoka Bunge, tulikipeleka kule tunaweza kufanya nini? Kukuondoa. Kwa hivyo hii ni nafasi mpya ya kuonyeshana kuwa Mbunge ni mtumishi wa watu awe Mbunge katika Baraza kuu la taifa ama kwenye baraza za wilaya ama baraza la kijiji.

William, habari ya access ya mjengo, vile watu wamefanya ndio warekebishe hiyo …Katiba ikija wakati itakuja itawapatia nafasi na muda fulani ukiwa hujafanya lenye linalotakikana nikija hapa nikiwa lazima nisaidiwe, unaweza kuenda kwa ofisi na ulipwe damages. Habari ya kuinuliwa sio habari ya matembezi ya kawaida. Kwa hivyo watapatiwa nafasi fulani kurekebisha mijengo na hiyo nafasi tushaandika unaweza kuenda kotini kushtaki, unaweza kushtaki koti ikiwa pia hawa hawajarekebisha nyumba zao. Itakuwa muda gani, tumewapa Bunge miaka miwili watengeneze sheria zenye zitahakikisha watu kuangalia habari za haki za binadamu na haki za walio na ulemavu ni kwenye haki za binadamu.

Habari ya materials, ni kweli kuwa kuna mambo mengi yenye itatakiwa kufanywa hapa kama ya kutoshwa kwa ushuru na nini lakini kuna haki. Kuna sheria mara tatu ama viwango tofauti za sheria, sheria ya Katiba ni mwelekeo, general principles ile kubwa. Sheria ya utekelezaji kuna nafasi zake mbili, ya kwanza ni ile ya kubuniwa na Parliament kwa hivyo Parliament ndio itasema kama serikali inawasaidia kuleta viombo na vitu gani venye wataitaji, moja ya kuraisisha itakuwa pengine kuwapa bure ama kutotoza ushuru ili wakaweza kununua na mambo kama hayo. Hiyo ni sheria ya utekelezaji na hiyo itafanyiwa na Bunge. Kuna policies, wakati fulani tutahitaji kuwa tunatenga ya ulemavu, the policy of disability na hiyo pia itaeleza habari ya utekelezaji wa ….(Inaudible). Kwa hivyo wakati huu pahali tuko ni principles, ikiwa tumesema una haki ya kuwa facilitated hiyo inakuwezesha kuenda kotini kusema mimi nina gari yenye naweza kutumia naweza kuendesha kwa mkono, nimetozwa ushuru na sijasimamiwa na Katiba inasema kuwa serikali itamwezesha kupata nini? Mambo yenye itanirahisishia mwendo wangu ama viombo venye vitanirahisishia mwendo wangu. Katiba inakupa nafasi willful ya kuanzia, leo huwezi kufanya hivyo kwani Katiba haijasema na ukienda mtu atasema hiyo ni Tume ya Katiba ya leo haina lolote pia kuhusu hiyo. Kwa hivyo sio sheria lakini kama imepumzika kidogo halafu sasa itatambuliwa kwa sheria za Bunge na sera zenye zitaanzishwa. Hiyo ndio mwisho wa maswali yenye nilikuwa nimeulizwa ya kwanza, kuna swali ambayo sijajibu.

**John Kariega:** Nafikiria yangu bado.

**Com. Salome Muigai:** Gani, nilianza na maswali yako what happened?

**John Kariega:** Swali langu la kwanza yenye niliuliza.

**Com. Salome Muigai:** Okay, wacha nitafute maswali lako. Niliandika kwa kalamu halafu hiyo kalamu ikakataa kuandika nikaenda kwa kalamu nyingine. Okay, John Kariega kutoka Kapsoya na swali lako la kwanza lilikuwa la mia moja na sita juu ya members of the National Council elections. Juu ya hii tumepeana mwongozo, kutakuwa na Bunge itaunda sheria za utekelezi lakini kwa kifupi ni kuwa members au kila wilaya itachagua mtu mmoja si hivyo? Kwani hii ni kusema hakuna kodi ….na kile na kingine kwa hivyo hii Bunge haitakua ya kisiasa itakuwa kazi ya ni kuangalia masilahi ya watu wa wilaya fulani fulani kwenye kikao cha kitaifa. Kwa hivyo haitakuwa ati huyu ni wa KANU na huyu ni DP na kila mtu akiwa ametoka Trans Nzoia tumempa watu jukumu fulani ,kutoka Uasin Gishu na pia tumempa jukumu fulani.

**John Kariega:** Atachaguliwa na wenyeji wa Bunge lipi?

**Com. Salome Muigai:** Wa Uasin Gishu.

**John Kariega:** Kwa votes.

**Com. Salome Muigai:** Yes, kwa votes, atakuwa elected atasimama na wakisimama watu kumi ama ishirini ama tano ama nne na mtamchagua. Na kila province kitachagua akina mama wanne pia hawa watachaguliwa na Nairobi itachagua akina mama wawili, kazi yao ni ya kuwakilisha …akina mama watakuwa na wajukumu kubwa watashinda mipaka ya wilaya na kuzungumzia habari ya province kwa jumla.

Constituencies ama vikao vya Bunge vitaanziwa kila baada ya set time, kila miaka kumi tutaangalia watu wa constituency na kuangalia kama tutahitaji kurudia mipaka ya constituency. But, kwa mpangilio huu mpya wa mixed member proportions yenye nilikuwa nimeanzisha sijuhi kama ulikuwa hapa wakati nilizungumza juu yake, uchaguzi wa chama. Wale watu wengi watapata viti ziadi kwa miji yao mradi tu wapige kura kwa hivyo Uasin Gishu ikiwa ina watu milioni moja for example na wapige kura wote na tuna upande mwingine yenye watu elfu ishirini it is proportional kuwa watu wa Uasin Gishu na chama chao watakuwa na viti vingine za ziada nyingi kuliko wale wachache, si hivyo? Kwa hivyo hivi ndio vile watafaidika, hata tukiangalia mipaka tena wale watu wengi bado wataweza kuhusushwa zaidi kwa wingi wa kura zao. Sasa tutapata maswali mengine kumi …

**John Kariega:** Nilikuwa nimuliza habari ya…

**Com. Salome Muigai:** Ulikuwa umeniuliza tayari?

**John Kariega:** 233, ndio nilikuwa nimeuliza.

**Com. Salome Muigai:** 233, public land. Tulisema kuwa wakati hii Katiba itakuja kuwa in place tutakuwa pia na Tume ya mashamba. Kwa hivyo ingawa kila mtu mwenye shamba lake binafsi itakuwa ni ya binafsi, lakini pia itachunguzwa vile ilivyopatikana. Ukiwa ulinunua shamba lenye lilikuwa limeibwa hili Tume itatupatia mapendekezo vile tunaweza kupata hiyo shamba tena kama lilikuwa limeibwa kutoka kwa uma. Hali nzuri ya shamba ni kuwa hata ukiiba uwezi kuiondoa pahali iko hata nyumba kubomoa sio gari yenye unaweza kuenda kuuza Uganda. Hata ukiniuzia shamba ikiwa ni ya Central Primary School na ukiuzia huyu mzee naye aniuzie na huyu auze, tutaaza kama mchotaji wa pesa. Kwa hivyo hata ukichota iwe kiasi namna gani ukitoa kwa idadi sijuhi kama you men know this. Nyinyi mnajua kushika ….(Inaudible) Ukishika hizo pesa itarudi mpaka wapi, mpaka pale ilianzia. Kwa hivyo hata ukiuza hilo shamba itaweza kutambuliwa, itarudishwa pahali lilitoka mpaka mwisho. Wewe mwenye uliuza ulikuwa umeuziwa na nani, wewe wa kwanza it can be done bora tuwe na political will. Hakuna jambo lilioundwa na mwingine yenye haiwezi kufanywa nini?

**Audience:** Kusuluhishwa.

**Com. Salome Muigai:** Kusuluhishwa. Basi haya ni maswali yenye nilikuwa nimewacha. Sasa nitachukua mengine sita ama kumi halafu nitafunga huu mkutano tafadhali. One, two, three, four, five. Kwani wewe siku….(Inaudible).

**Speaker:** Kuna huyu.

**Com. Salome Muigai:** Kuna jambo lengine ningetaka kusema hata kabla sijaulizwa swali na huyo mama msichana. Kuwa lugha zetu za Bunge tumesema Kiswahili na Kiingerezana Sign language, tumeongeza kama ishara. Tumeongeza pia kwa maandishi yetu, tutaandika kwa Kiingereza, Kiswahili na kwa Braille hata kabla sijaulizwa maswali mengine. Lakini ni lazima watu wasome hii Katiba ndio wasiniulize maswali yenye tayari iko hapa. So can I have the first five people? Watu watano wenye nimeita kujeni mbele. Tafadhali ongea kwenye microphone kwani tunafanya recording ya mambo hayo yote.

**Tobia Otunge:** Ninaweza kuanza.

**Com. Salome Muigai:** Yes na utuambie jina lako na uweke mic karibu na mdomo.

**Tobias Otunge:** Okay naitwa Tobias Otunge. Swali langu la kwanza linahusu mambo ya uongozi wa viama.

**Com. Salome Muigai:** Tulikubaliana tuma mikutano mingapi?

**Tobias Otunge:** Okay, swali langu la kwanza linahusu uongozi wa vyama. Nafikiri vile tunavyojua hadi wakati huu kwamba no public servant anakubaliwa kuwa official wa chama chochote na sijui kuwa mnajua kwamba ukitaka kuingia kwa siasa lazima ujiuzulu. Lakini hapa nikiangalia kifungu cha mia moja naona kwamba mtu yeyote ambaye anataka kuwa Rais ama mtu yeyote ambaye ako na cheo cha deputy secretary anaweza kuwa official wa chama. Je, huoni ya kwamba mtu akiwa katika government na akiwa official wa chama si anaweza kutofanya kazi yake vizuri kwa sababu pengine ikiwa haweza kupata nafasi ama masaa fulani na mimi ni official wa chama fulani nitaweza kuwa naweza kuwa deployed ili hata pengine nisilete …(Inaudible)

Swali la pili ni kuhusu mambo ya hukumu ya kifo, ningetaka ufafanuzi ni vipi mlipendekeza ya kwamba hukumu ya kifo iondolewe kwa sababu naona ingawaje kwamba mtu hawezi kuuwa akiwa hai lakini sioni vile mtu anaweza kuuwawa kwa sababu ikiwa mtu ana lengo na amefanya …(Inaudible) Isiwe kwamba anaua na huyo mtu apewe life imprisonment…(Inaudible). Kwa hivyo nafikiri hata Amerika ambayo ni nchi ambayo ni ya demokrasia bado imekataa death sentence kwa mimi sijuhi kama ni maoni ama ni swali lakini nimeizungumzia hivyo.

Nafikiri niko na nyingine hapa kuhusu national days, nikiangalia kwa hiyo draft naona kwamba sijaona Moi Day, sijaona Kenyatta Day. Those are the two national days kwa hivyo nataka ziwe za taifa. Mimi naona hamgetoa those days na mmebakisha lakini mnge…

**(Interjection)**

**Com. Salome Muigai:** Tafadhali tunafanya recording na tungetaka kuwa na mambo yenye inaweza kusikiswa. The reason why tuliweza kabisa kuandika maoni yenu ni kwani tuliweza kuyasikiza tena tukiwa Nairobi. Watu wenye walikuwa kwenye hiyo mikutano itabidi kusikiza na kuyaandika na pengine hata hatukuambia kuwa leo tumeleta maoni maoni yenye mlitupatia katika Eldoret East Constituency, tunayo maoni yote yenye ilitolewa kwenye constituency. Tuliyatoa kwenye recording, kwa hivyo mkipiga kelele mwenye atapatiwa hii tape ili aiandike atakuwa na shida kabisa.

**Tobias Otunge:** Okay, nilikuwa nikiuliza kuhusu national days na nimesema nimeona ya kwamba Jamhurii na Madaraka tumepatiwa lakini hatuna Moi Day and Kenyatta Day. I don’t want to talk about Moi Day kwa sababu pengine hiyo inaweza kuwa jambo tofauti lakini Kenyatta Day inatukumbusha mengi. Vile tunajua kwamba nikiwa mahali ilikuwa katika wakati za uhuru ingawaje napendekeza badala …tunge I-rename kutokana na the objectives and virtures of that day as highlighted rather than resorting to giving it the name of an individual but it should be retained and be renamed.

Lastly, sijuhi kama hii itakuwa ni swali lakini nauliza kwamba kuna wakati ambapo nimejaribu kuenda through the draft lakini kuna wakati nilisikia mzee, our President akisema kwamba kuna mambo ambayo yako katika Katiba ambayo hata huwezi

kusema mbele ya watu sasa sijuhi kwa sababu nimeenda through lakini sikuona mambo siwezi kusema mbele ya watu.

**Speaker:** Hiyo ni maoni.

**Tobias Otunge:** Kwa hivyo pengine wanaweza kutueleza kama kunayo. Thank you so much.

**Com. Salome Muigai:** Endelea mama, anza na majina kamili tafadhali.

**Beatrice Gashube:** Majina yangu ni Beatrice Gashube.

**Com. Salome Muigai:** Beatrice who?

**Beatrice Gashube:** Gashube. Swali langu ni maswali limeguziwa kidogo na ilikuwa ni juu ya kifo Kitabu imesema ya kwamba kila mmoja ana haki ya kuishi na ikaondoa hukumu ya kifo. Basi ningependa kuuliza suluhisho itakuwa ni nini kama hatutakuwa na hukumu ya kifo. Hukumu hii ya kifo ilibadilishwa na badala yake ikawa nini? Na swala lingine mama nilikuwa nauliza wenzangu wametaja.

**James Soi:** Asante sana. Mimi nina swali moja hapa na inatoka sehemu ya land ownership.

**Com. Salome Muigai:** Tupe majina kwanza.

**James Soi:** Jina ni James Soi. Kwa hivyo kwa ownership of land kipengele nambari mia mbili thelathini na mbili. ….. swali naulizaje, hiyo ndio swali la kwanza.

**Com. Salome Muigai:** Swali lingine, hiyo ndio ya mwisho ama ulikuwa na nafasi tayari. I thought you were number five.

**James Soi:** Right.

**Com. Salome Muigai:** Okay, not tha I have any problem women aspects but I would like to see more of you.

**Samuel Cheptorus:** Madam Commissioner and marafiki zetu…..

**Com. Salome Muigai:** Jina lako baba.

**Samuel Cheptorus:** My name is Samuel Cheptorus.

**Com. Salome Muigai:** Endelea.

**Samuel Cheptorus:** This is the question and it is touching on the question of….and I would like you to be more elaborate on election of village, location and district councils. May I therefore take this opportunity in my own capacity and ask the same question whether these elections are to be held together with parliamentary and presidential elections. Asante.

**Grace Cherotich.** Kwa majina naitwa Grace Cherotich ama mama Rai. Niko na maswali mawili na oni moja kwa niaba ya wakaaji wa hapa Eldoret East. Swali lango la kwanza ni kuhusu watoto, children with special needs kama with facilities, street children and other children.

**Com. Salome Muigai:** …(Inaudible)

**Grace Cherotich:** Kwa hii Katiba inayopendekezwa hapa inaonyesha kwamba watu wanahitaji kulindwa na State na society sasa sijuhi itakuwa vipi, ni kama sielewi mimi kwa sababu sana sana kama ni ya serikali ama raia inakuwa hapo kati kati. Kwa sababu sitaki kuwa ya raia na tena iwe ni serikali. Sasa ningependa kama ifafanuliwe kabisa kwa sababu itawekwa Commission ya ku-deal na maneno ya watoto ama kitu kama hiyo ingawa watoto wasaidiwe sana sana hawana makazi hata tuna wale …(Inaudible)

Halafu ya pili ni kuhusu family, sikuelewa kama hapa mkisema family mnamaanisha nini halafu nikisoma hapo chini mnasema mtoto ako na right ya kulindwa na baba na mama. Kuna families ambao wako hivi sasa kabla ya hii Constitution kuja kutumika ambao wako na mama peke yake ama wako na baba peke yao, sasa ikifika kwa hii family watawekwa hapo kama family ama watafanyiwa namna gani sana sana wamama, single mothers.

Swali lingine la tatu halafu nitaongeza ombi moja ni hii ya nomination of MP's hii sikuiona hapa na sijuhi kama iliwekwa ama ilitolewa na kama iko mahali na sikuangalia labda Madam Commissioner atatufafanulia tuone. Kuna hii mambo walikuwa wanasema nomination of leo ni hivi nitakuwa niki….(Inaudible) tunataka kujua ukweli ama la. Na hivyo tena ilikuwa ni nzuri sana sana, unapata anapewa nomination mpaka mtu anapata viti vingi na pia anawekwa na President kuwa waziri na hawa….(Inaudible) kitu kama hiyo sijuhi kama itupiliwe mbali ama itafanyiwa namna gani.

Ya mwisho ni ombi kwamba tulifurahi kama vile tulipata hii draft Constitution ingawaje ilibidi tununue nadhani mki-print tunaweza kununua hiyo lakini mtu kujitokeza kwa sababu anataka kupata hii copy na kuangalia maneno yetu inaenda namna gani. So far it is good na tunaona delegates wetu watatu kufikisha mambo mengi yenye tumesema hapa. Sasa ombi langu ni kwamba ikishafikishwa tutapata aje copies za hiyo final Constitution, mfanye arrangement kama commission muone vile….

**Com. Salome Muigai:** …(Inaudible)

**Grace Cherotich:** Okay sasa nilikuwa naomba hivi ikiwa final Constitution lazima itaandikwa kwa vikaratasi vidogo na sana sana nchi yetu imekuwa Commission ikimaliza kazi, hiyo Constitution inatolewa na inawekwa kwa drawer. Sasa tunakuwa hatujuhi haki yetu iko wapi, hapo tunaona imekuwa kazi ngumu lakini nisipopata final document ya hii sitajua vile nitafanya. Kwa hivyo naomba mfanye mpango ili kila raia apate copy ya hii Katiba na kukaa nayo. Asante.

**Rosemary Chepkorir:** ***(Deaf, through translator).*** Majina yangu ni Rosemary Chepkorir kutoka hapa Eldoret nimesoma kwa chapter five katika page 134 na nimeona kwamba sign language imekubaliwa kwa Parliament pamoja na Kiswahili na Kiingereza lakini kwa colleges sioni kama wameweka kwa colleges hata university na huko ndio mahali tutaenda tukimaliza form four lazima waende university which means imesahaulika hapo. Kwa sababu tunaendelea na baada ya college tunaenda kufundisha watoto wetu wale hawasikii. Anataka hata TSC to consider them kwa mambo ya uwaalimu. Asante.

**Com. Salome Muigai:** Asante kwa maswali hayo, hayo ni maswali mazuri naona kila mtu anasikiza kwa makini. Tobias anauliza juu ya ile siku ya viongozi wa viama, tulisema kila mtu ana haki ya usiasa. Nafikiri tumepatia kila mtu haki ya kuwa mwanasiasa ingawa tu haki yaki kudhulumi kazi yake. For example una haki ya kidini si hivyo? Ukiwa Adventist na wewe ni Mkatoliki na si adventist unawacha shule yako kuhudumia habari ya dini ya Adventist, no si bado unafanya jukumu zako pamoja na dini yako. Ndio pia tunataka siasa yetu iendelee kuwa iwe sio siasa yetu iendelee kukua iwe sio siasa itakutukataza, sio siasa ya kubomoa ni siasa ya kujenga. Ile mambo yenye inatugenganisha na tunaendelea kuzingatia tofauti zetu hiyo sio mambo ya kujenga ni mambo ya kubomoa. Mambo ya kujenga inazingatia umoja wetu na ile mambo yenye mtu amepatiwa jukumu ya kufanya au pia ukiwa wewe ni Muislamu na unafundisha shule ya kawaida na ijumaa ndio pia uko na wakati wa kuenda kwenye laboratory lako kufundisha chemistry siku ya ijumaa, unajiacha na uende Musikitini? Si, unaendelea na ukienda kufundisha chemistry unaleta dini yako hapo? La. Sisi Wakenya tunajua kugawanya utaalam wangu na mambo yangu ya kibinafsi. Kwa hivyo tunataka kupitia wakati wenye siasa zangu hazitanikataza kufanya majukumu yangu na ndio vile pia tunasema kabila langu lisinikataze kufanya huamuzi wangu. Kwa mfano kwenye hii Katiba nina haki ya kuzungumza lugha ya mama lakini kama mimi ningekuwa nimetoa hiyo mafunzo yote na Kikuyu watu wangapi wangeelewa? Inua mkono kama ungeelewa Kikuyu, watu watatu mnaona? Kwa hivyo nina lugha ya Kikuyu ndio, nina haki zangu lakini hiyo hainikatazi kuelewana na Mkisii ama kuongea lugha yenye itatueleweka kwenye Mkisii, Mkalenji, Mjaluo na kwa Mkenya yeyote anahitaji kufikiwa na maneno yenye tunazungumza. It is a maturity, it has to be reached, it is a devolution of maturity. Wakati huo tukifika hapo tutaweza kulinganisha majukumu wetu na haki zetu.

Shida ya death penalty watu bado wana shida na kuwa na hiyo hata mtu mwenye ameua kwa nini afungwe maisha bado tu watu watafungwa maisha, ukiwa umeuwa ama ulihitaji kuuwawa Katiba hii ikianza kufanya kazi kila mtu mwenye alikuwa anangoja kuwawa atafungwa maisha. Lakini ikiwa pengine ungeuwawa kabla hii Katiba haijatolewa na ufungwe maisha hutakuwa na haki ya kuhurumiwa. Ni kifungo cha maisha na kukaa mpaka hiyo maisha itakapomalizika.

Siku za Kenyatta Day na Moi Day, hii tulizungumza kwa wakati mrefu sana tukiwa wanatume tulikuwa na debate yenye mlileta. Sana sana tulifukiria Kenyatta alikwa President wa hii nchi na pia President Moi amekuwa Rais wa hii nchi lakini sasa tumegeuza Katiba tukasema kwa Katiba ya sasa kuwa Rais atakaa kwa muda mingapi, miwili ya miaka ngapi?

**Audience:** Tano.

**Com. Salome Muigai:** Tano kwa hivyo Rais mwenye atakaa sana ni miaka mingapi? Kumi, kwa hivyo kwa miaka hamsini ijayo huenda kukawa tuna Rais wengine wangapi, watano na kukiwa kuna mmoja mwenye hatujamchagua tena, si zinaweza kuwa mara tano ama ile kumi. Sasa tukimpa kila mtu siku yake wananchi watafanya kazi lini na tutachaguaje mwenye tutapatia na mwenye tutanyima. Kwa hivyo hiyo ndio swali lenye lilikuwa kama inatutatiza kuwa ine the next 100 years tutakuwa na Raisi kumi ama ishirini, si kunawezekana tuwe na ishirini? Sasa hatutaweza kumpatia kila mtu siku yake lakini ikiwa bado watu wana maoni ya ziada na wangependa kuongeza hizo siku tafadhali patianeni maoni yenu yatajadiliwa kwenye kikao cha kitaifa.

Hii maneno yenye haieleweki kwa hii Katiba na haiwezi kuzungumzwa mbele ya watu hata mimi bado sijaiona kwani nimewapeleka sura kwa sura na hakuna pahali penye nimerukia kwani ilikuwa jambo lenye hatukuweza kulizungumzia na pia tulikuwa na watoto na akina mama kwa hivyo tungekuwa na shida. Basi hiyo sijaliona mimi. Lakini mwanzoni mwanzoni kulikuwa na pahali pengine palisema familia yoyote hiyo inaweza ku-propose, basi tukaona pengine hiyo italeta tashwishi kwani mila zetu za Kiafrika tunajua familia imeundwa na nani na nani. Lakini sio familia yoyote ile huenda ikatuletea shida, lakini hiyo maneno ilikuwa hiyo yoyote ile itakavyokuwa familia itakapokuwa imeundwa na tulikuwa tunasema hivyo zaidi kwa ajili ya single parents awe ni single father na single mother mwenye ana watoto ama yeye ako peke yake. Tungetaka hizo familia zote zipate heshima na usawa katika Katiba, mbali na hiyo sijaona jambo lingine. Na tulitoa pahali pa kusema vyovyote ilivyoundwa, tulitoa mapema kabisa.

James Soi on ownership of land, I would like to know if Kenyans will take care of the landless. Tulisema kuwa Tume hii yenye tumeweka ndio itachunguza habari ya ardhi na mashamba. Hii iko kwa akina nani, nani mwenye hana, inawezekanaje kupata distribution yenye itahakikisha kuwa kila Mkenya angalau ana nafasi ya kuweza kupata pahali pa kujenga okaishi na akaweza kufaidika kwa ukulima.

Samuel Cheptorus, elections ya different sections. Tulisema kuwa Katiba ni mwelekeo si hivyo? Kwa hivyo Bunge itaunda sheria zenye zitatulekeza vile watu tofauti watachagua eneo tofauti. Kwa wilaya nafikiri itakuwa kama ya Bunge lakini kwenye wilaya, kwa vijiji huenda watu wakafikiria vile watachagua wenyewe na kufuata sheria ya utekelezi yenye itakuwa imetoka Bunge na pia sera za uchaguzi.

Watoto wenye special needs, watoto wenye matakwa ya kipekee kama ulivyosema wasichana wakati mwingine wana matakwa ya kipekee kabisa na watoto walemavu na refugees. Tumewekelea hayo ili kuwe jukumu ni ya wazazi, kuna mzazi

mwenye anasomesha watoto wake isipokuwa yule mlemavu si ndio? Na sio kwamba hana mali, ni kuwa hakufikiria anataka. Kwa hivyo hiki kipengele kinalazimisha huyu mzazi kuwa watoto wake wanausawa moja mbele ya sheria. Lakini pia tumesema wakati wa serikali inataka kusaidiwa lazima hawa watoto wenye shida za kipekee nao wafikiriwe kwa ziada. Hauwezi kusema kuwa nimeshanunulia kila mtoto vitabu basi kila mtoto asome. Tulikuwa kukiwa kuna mtoto mwenye haoni lazima matako yake yafikiriwe ndio hivi kwenye hivi vipengele hasa habari ya ulemavu tunayo kwa Braille hata hapa hivi sijuhi kama ililetwa. Ukiwa una mtu mwenye unamjua anahitaji kusoma kwa Braille tumeleta kwa Braille kwa hivyo tumesema ingawa hizi nakali zimetolewa kwa print it is not enough yule mtu mwenye hawezi kusoma kwa nakala, kwa mandishi lazima apatiwe Braile. Kwa hivyo ikiwa hata ikiwa ni msaada wa serikali yenye itapatia watoto lazima watoto hawa wenye shida za kipekee kuangaliwa kwa ziada.

Family, tumezungumzia habari yake kuwa Parliament itaunda sheria zenye zitaonyeshana ufafanuzi wa familia. Habari ya nomination seats, zile zaidi zenye mliambiwa tumezungumzia kuwa chama chenye kitapata watu wenye kutupa viti vya ziada zitapata viti vingine, hivi viti ndivyo venye vile tisaini na tunasema nusu ya hivi viti vitaenda kwa akina mama ile Parliament ipate ile theluthi yenye Katiba inauliza. Hizo nusu nyingine zitaenda kwa walemavu, vijana, wataalam na watu wengi wenye watakuwa tunahitaji kwenye Bunge lakini hawakuweza kuwakilishwa na kura. Kukiwa na watu kama kabila ndogo kama Ogiek hata wakikaa miaka yote hawataleta Mbunge. Lakini sasa kwa hiyo mpangilio wataweza kupata kiti kimoja ama viwili walete watu wao ama Dorobo, ama watu wale wengine wa jamii zilizo ndogo, mnaelewa. Kwa hivyo hivyo viti ni za kila mtu si tu kusema ati ni viti vya nomination, ni viti vya kuleta diversity ya nchi kwenye Bunge ili sura ya Bunge iwe sura ya Kenya.

Tukimalizia hapo Constitution italetwa kwenye shule, kwenye library iliyo karibu na wewe, kwenye ofisi za serikali, kwenye Makanisa na kwenye Musikiti ili kila mtu apate nafasi ya kuiona Katiba kwa ofisi iliyo karibu naye. Na pia zaidi tutafsiri. Itaweza kuuzwa lakini itauzwa kwa bei nafuu ili kuhakikisha kuwa kila mmoja akiitaji anaweza kujipatia nakala yake. Kama Bible inauzwa na kila mtu anaweza kufanya kazi mpaka akaweza kununua lakini hii itaweza kuuzwa kwa bei nafuu.

Sign language in colleges, tumefurahi sana kuwa sign language tayari imefika kwenye Katiba ingawa haijafika kwenye Bunge. Bunge ndio yenye inaleta lugha zilizo rasmi, ndio tekelezi ya lugha zilizo rasmi. Kwa hivyo pia tuna lugha ya ishara kwenye Bunge ni kuonyeshana imelindwa kama lugha rasmi na sasa itahitaji sheria zingine za kutoka Bunge na kutoka kwenye sera za taifa kuipeleka lugha ya ishara pahali pengine popote kama mahakamani, polisi, shule na pahali unaenda kumwona mtoto wako na pahali pengine. Lakini ni vizuri kuwa kwa mara ya kwanza Katiba inasema lugha ya ishara ni lugha yenye itatambulika katika nchi ya Kenya na pia lugha ya maandishi ya Braille.

Asanteni sana nataka kuwashukuru kwa utulivu wenu mkubwa na tumefunga kikao hiki ukitaka swali sasa utaniuliza moja kwa mwingine na ningetaka kwa uvumulivu wa kutungoja leo asubuhi na kusema wakati unaposikia kuwa habari ya Katiba inakuja Uahin Gishu tafadhali njooni kwa wingi. Sisi ni watu wengi katika eneo ya Uasin Gishu District. Tulipoenda Kitale Town kulikuwa na watu mia tano kwenye hall, tulienda kwa hall ya museum. Tulipoenda Cherengany kulikuwa na watu 400 na Kwanza mia tatu na hamsini. ASK show tulipoenda hapa Eldoret, tulipokuwa tuna mkutano pale Show Ground tulipata watu

tisaine na nne na kati ya Kitale na Eldoret gani kubwa?

**Audience:** Eldoret.

**Com. Salome Muigai:** Leo sijuhi nina watu wangapi lakini hatujafika mia mbili. Kwa hivyo kuna shida na watu wa Uasin Gishu tafadhali tujitokeze kwa dhati, hii ni Katiba yetu. Tutafanya election mwaka huu na mwaka ingine ikija tutafanya nini. Tutafanya elections? Si hivyo mara nyingi. Lakini Katiba tutapata nafasi ya kutengeneza hivi karibuni? La. Kwa hivyo hili ni jambo muhimu na tungetaka kukueleza wewe ukienda tafadhali watu wa Eldoret mna mkutano mwingine kesho na tafadhali waambie watu waje ili tuweze kuelewa Katiba hii mpya inasema nini.

Asanteni sana na Mungu awabariki. ***(Applause)***

**Gilbert Bor:** Asante sana Madam Commissioner.

**Com. Salome Muigai:** Ikiwa kuna mtu mwenye angehitaji kusoma kwa Braile tafadhali chukua nafikiri kadhaa.

**Gilbert Bor:** Ningependa kushukuru Madam Commissioner na wote ambao wamehudhuria mkutano wa leo na sasa ningependa kutangaza kwamba baraza ya kufanya launching leo kwa Eldoret East ya draft Constitution tumepanga sasa ya mashinani. Tutakuwa kwa Kaptagat Division tarehe ishirini na moja, Jumatatu, tutakuwa Laiben Centre ya kueleza watu wetu hii draft kwa watu wa location za Kaptagat, Beliomo. Kwa hivyo kama kuna watu wa kutoka sehemu hiyo waambie watu wengine kwamba tutakuwa na mikutano. Siku hiyo hiyo tarehe ishirini na moja tutakuwa na mkutano mwingine Chepkrumo Centre na hiyo itajumuhisha watu wa Kipkavo na Chepkoroi Division.

Halafu tarehe ishirini na mbili mwezi huu, Jumanne tutakuwa na mkutano katika Kapsoya Secondary School ambayo itajumuhisha watu wa Kapsoya Location na vile vile watu watangaze hiyo sana. Vile vile tarehe ishirini na mbili tutakuwa na mkutano Burnt Forest ambayo itajumuhisha watu wa Burnt Forest area na Olare Location kwa jumla. Tarehe ishirini na tatu tutakuwa na mkutano Eldoret Polytechnic ambayo itachukua watu wa Lasho na vile vile….. Halafu siku hiyo hiyo tutakuwa na mkutano huko Ainapkoi ambayo itajumuhisa watu wa Ainapkoi Location na Kapng'etuny, hiyo ni Ainapkoi Division.

Katika Moiben Division tarehe ishirini na moja tutakuwa na mikutano mbili. Moja itakuwa kwa Chief's Office, kwa watu wa Moiben Division na Kuisoro Chiefs Office kwa watu wa Mashimoni Tembelio na Kuisoro Location. Halafu tarehe ishirini na mbili tutakuwa na mkutano wa watu wa Kandolo Location kwa Kandolo Chief's Office, tarehe ishirini na nne vile vile tutakuwa na mikutano miwili moja itakuwa Moiben Town na itajumuhisha watu wa Moiben Location na Mumukei Location. Ya pili itakuwa Chepkagas Chief's Centre na itajumuhisha watu wa Chepkoi Location na Chepkoilel Location.

Hiyo ndio orodha ya mashinani katika Eldoret East na watu ambao wameudhuria pia wapeleke habari hizo na wapange mikutano ya vijiji vilivyo, kwa sababu madhumuni ya hii draft Constitution ni kupatia nafasi watu wote kujadiliana, tu-debate and tu-discuss na kutoa maswala ama maswali kama yalo ambayo yaliulizwa hapa. Kwa sababu National Conference itaanza very soon tarehe ishirini na nane ukija katika Documentation Centre ya Uasin Gishu tutangojea tupokee recommendations zenu ili tuwakilishe katika national office ipelekwe kwa National Conference. Kwa hivyo mkiwa na maneno yoyote ambayo ungetaka kuchangia kurekebisha the draft ni jukumu lenu mliandike kwa maana hatutakuwa na nafasi tena. Muandike na mlete kwa ofisi yangu na mimi nitahakikisha kwamba zimepelekwa Nairobi.

Ningependa Madam Commissioner although…..(Inaudible) mzee unaona katika Katiba mpya tunazungumzia maneno ya National Council, huyu mzee alikuwa Senator ya serikali ya kwanza.

**Mark Daliti:** I will just say a word. Thank you very much Commissioner and the rest. My name is Mark Daliti, Senator Uasin Gishu North from June 1993 up to April 1966. When I lost in a by election because of KPU, Kenya People's Party I have been trying again but now I am old but if I am given a chance I have five years to go, ***(Laughter)*** untill when I will be unable to talk, thank you very much, endeleni. I am going to write my recommendations. (***Applause)***

**Gilbert Bor:** Huyo alikuwa Senator wa Uasin Gishu kabla ya Senate kuvunjwa. Wakati senate ilivunjwa ndio mnasikia kutaka kwake, aliingia KPU tena na mnajua mambo ambayo iendelea.

Madam Commissioner ningependa tena kuchukua nafasi hii tena niwasimamishe wale District Delegates ambao wako hapa tuwajulishe wale walikuja late ili wajue nani anaenda kuwakilisha wao.

His name is Julius Sietenie, Emmy Kiprop, hawa wawili, Emmy Kiprop na Julius Sietenie kuna mwengine wa tatu Bwana Keter nafikiria atakuwa kwa mikutano ya Eldoret North kesho na Bwana Samuel Tororei ndio wanaenda kutuwakilisha sisi watu wa wilaya wa Uasin Gishu katika National Conference. Kwa hivyo maoni yote ile mtatoa tutatuma Nairobi na hawa ndio watashugulikia, tutatuma kwa headquarters na tuwapatie copies na ninatumaini kwamba watatetea matakwa yenu. Asante sana.

Vile vile ningetaka kutambua the presence of some of the people who worked with us during civic education. Tafadhali , ni nyinyi wawili tu? Kulikuwa na wengine. Basi hawa wawili njooni mbele halafu mtaje majina yenu ili watu wapate kuwajua. Na hawa pia tutashirikiana nao katika hio mikutano ambayo nimetangaza.

**John Kariega:** Asante District Coordinator, kwa majina yangu ni John Kariega wakati wa kufunza elimu ya jamii nimekuwa nikishirikiana na ofisi yake na kwa kweli tumetembea na nina furaha nyingi kuona ya kwamba yale yako katika draft hii mengi ni yale yalitolewa na watu wale ambao tuliwafunza. Asanteni.

**Mathayo Ranja:** Coordinator, Madam Commissioner mimi jina langu ni Mathayo Ranja mimi ni wa hapa maana mimi ni mtu wa Eldoret North Constuency na zaidi ya hayo tumefanya kazi hii pamoja na mwenyekiti wa Uasin Gishu katika jumuia ya kanisa, NCCK. Asante sana.

**Ruth Mwema:** Asante sana. Kwa majina naitwa Ruth Mwema mimi nilikuwa nasaidia kwa civic education na ninashukuru kwa sababu kwa upande wa akina mama tumepewa masaa mingi sana hata …(Inaudible). Asanteni.

**Zakayo Sifuna:** Madam Commissioner, District Coordinator na wakilishi wote hamjambo?

**Audience:** Hatujambo.

**Zakayo Sifuna:** Kwa majina naitwa Zakayo Sifuna mwenyewe ni wa Eldoret North lakini pia niliweza kuona nifike hapa leo nilikuwa hata Show Ground kwa hivyo nafikiria nimefaidika sana kwa mawazo kutoka kwa Madam Commissioner na nitafika mashinani kuweza kujulisha wengine. Kwa hivyo asanteni sana.

**Joyce Wanjiri:** Asante Madam Commissioner na wasikilizaji, kwa majina yangu ni Joyce Wanjiru Kamau mimi nimetoka Kapsoya ama …..na nimeweka kufanya na Mr. Bor ku-mobilze akina mama na upande wa Kapsoya Location niliweza kuwa-mobilize na ninashukuru kuna mambo mengi sana nimeona yame-appear hata ingawa iko moja ambayo ilikuwa tisho langu sana. Madam Commissioner ningesema ya kwamba katika hii maoni ya Constitution sijaona hiyo jambo ikiwakilishwa na hata kama nitaona Madam uli-mention tu kidogo. Katika nchi yetu tunaona kuna generation moja ambayo iko kati kati na ni tisho kwa kila mtu na hiyo generation ya watu wale tunaita hawkers, sijaona pahali Constitution ime-mention hao watu na mnakubaliana na mimi hiyo generation ni tisho kwa kila mtu. Asante.

**Gilbert Bor:** Asante sana Mrs. Kamau ametusaida sana kweli kwa mobilization hata district pia zaidi ya hiyo yeye ni mwalimu na ni mwakilishi wa waalimu katika sehemu hii. Vile vile..

**Com. Salome Muigai:** If you mobilized them where are …(Inaudible).

**Gilbert Bor:** Vile vile Madam Commissioner ningetaka kutoa shukrani kwa our colleagues …(Inaudible). Vile vile nashukuru Bwana …(Inaudible)
I would like to invite the person who will lead us in the closing prayer.

**Com. Salome Muigai:** Ningetaka kushukuru sana watu wenye wamefika na asante sana kwa kumsaida Bwana Coordinator lakini ningetaka kusema kuwa tukihusisha watu wakati yenye tukipika kama sisi akina mama, sasa ni wakati wa kukula chenye

tulipika lazima tuwahusishe watu hao wote wenye walikuwako wakati wa kutengeneza. It is very very crucial that people get to hear about this Constitution and they get to see it and they get to own it. It is good that you mobilized for people to come and give out their views but it is equally important in fact more important that they can critic, not necessarily critisize this document especially women. Akina mama nasikia mlisema mlileta akina mama na leo tunataka theluthi moja sasa hata tungepatiwa theluthi moja hapa we would not get enough people to take the seats. Ndio unasikia nikikuwa challenged by the men. So please and even the men themselves this is a very small number for such a big town. So we need to pass the word to others, I hope that there will be more people tomorrow for Eldoret North. Where will be meeting be?

**Gilbert Bor:** The meeting will be here.

**Com. Salome Muigai:** So the meeting will be here please tell others to come. Thank you very much.

**Gilbert Bor:** Basi ningependa kuita mtu wa kutupatia maombi ya mwisho.

**Prayers:**

Tusimame wote ili tuombe. Mungu Baba tuko mbele yako tukitoa shukrani zetu maana Mungu Baba umekuwa kiongozi na Baba tunakubali ya kwamba umekuwa pamoja nasi tungu mwanzo na ndio maana tunaweza kumaliza majadiliano bila shida yoyote. Baba tunaomba ikaweza kuwafikia wale wote wakiendelea kushauriana na hata wale wanataka kuenda Nairobi, Bana tunaomba Roho wako Mtakatifu akaweze kuwa mwalimu wao, akaweze Mungu Baba kuwapa upako wa Roho Mtakatifu kwenye vinywa vyao ili Baba wakaweza kunena yale yote ambayo yatatufaa sisi kutoka wilaya hii ya Uasin Gishu ili Baba tukapata kuandika mambo ambayo yatatusaidia na vizazi vijavyo. Baba tunashukuru, tunaomba hata wakati huu ambao tumeendelea kuelekea kwenye uchaguzi mkuu Baba tunashukuru ukaweze kutupa amani katika umoja na katika upendo ili Baba wetu wa binguni tuweze kuwa pamoja nawe katika nchi hii yetu ya Kenya. Maana Mungu Baba tunajua ya kwamba Roho wako Mtakatifu haishi malala ambapo hakuna amani, ndiposa Baba tunaomba hivyo vitu ili Baba sehemu hii yetu iweze kuwa makao maalum ya roho wako mtakatifu pamoja na jeshi lako la binguni. Baba wetu we binguni tunaomba hata pahali wa wanenaji hawa Commissioners ambao wanaendelea kudhuru mahali tofauti kila wakati Baba ukaweza kuwapeleka salama wakati huu na sasa ninaomba pahali katika kazi zao Baba uwape nafasi njema, uweze Baba kuwaondolea shida zote za muovu shetani ili wawezi kuwafikia watu wengi na wakaweze kupata mawaidha kutoka kwa wao na hata pia kuwapa mawaidha. Baba tunaomba ili kwa ajili ya serikali pamoja na hata waalimu ambao wanagoma, pamoja hata na wanafunzi na waalimu baba ukaweze kutupea suluhisho wakati huu, suluhisho ambao Baba linaweza kuleta mzingi wa upendo ili wakaweza kujua upendo wako na hata kupenda kukutumikia. Baba tunaomba hata tunapoondoka kuelekea kwetu Baba wetu wa mbinguni uweze kutukinga na shetani muovu na hata tufikapo kule tunaenda Baba tutakushukuru na tutalimidi jina lako maana tunaomba tukiamini katika jina hilo safi la Yesu Kristo.

**Audience:** Amen.

**The meeting ended at 4.35 pm.**

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**